epaper.ippmedia.com
Nipashe MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Nipashe JUMAPILI

Jumapili Desemba 15, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • No. 0581891
www.twitter.com/nipashetz
www.ippmedia.com
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
0677 020 710
LIKE & FOLLOW US

UKURASA WA 2

**Dira** ya Maendeleo yaweka kipaumbele Katiba mpya imara



UKURASA WA 5

**Madini** ya vito kuuzwa kidijitali kuongeza uwazi

UKURASA WA 11

MAISHA YALIVYO

**Hiki** ndicho chanzo cha matatizo ya ndoa nyingi



UKURASA WA 22

**Mbappe kusafiri na Madrid Qatar**

## RIPOTI MAALUM

# Wenye uvimbe kwenye uzazi wasimulia mateso wanayoyapata



UKURASA 4



Rais wa Zanzibar, ambaye pia ni Msarifu wa Taasisi ya Benjamin William Mkapa (BMF), Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimkabidhi nyenzo za kufanyia kazi Mwenyekiti mpya wa Bodi ya Wakurugenzi ya taasisi hiyo, Balozi Liberata Mulamula, baada ya kuizindua bodi hiyo jana katika ukumbi wa jengo la BMF, Kawe mkoani Dar es Salaam. **PICHA: IKULU**

# Siri Wachaga kurudi kwao mwisho wa mwaka yaanikwa

UK. 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 24

### SIMBA SC YATAMBA CS SFAXIEN 'ITAKUFA'



KATIKA kuhakikisha wanazipata pointi tatu nyumbani, Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, ameahidi kubadili mfumo ili kuwafanya wachezaji ...

# Bei vyakula hazishikiki kila mahali, sababu hizi

UKURASA 3

**MICHEZO** DUBE AIBEBA YANGA CONGO UK.24

**MAONI,** UK.6

HABARI KITAIFA

# Dira Maendeleo 2050 yaweka kipaumbele katiba mpya imara

**Na Restuta James**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji), Prof. Kitila Mkumbo, amesema Dira ya Maendeleo 2050, imeweka kipaumbele cha katiba imara yenye mwafaka wa kitaifa, demokrasia na mfumo madhubuti wa vyama vya siasa.

Aidha, amesema inataka pato la Mtanzania lifikie Dola za Marekani 4,700 (takribani Sh. milioni 10), kutoka dola 1,210 (Sh. milioni 2.8) la sasa; na la nchi lifikie Dola za Marekani bilioni 700 (Sh. trilioni 1.5).

Aliyasema hayo Dar es Salaam jana wakati wa kikao cha Tume ya Mipango cha maoni ya uhakiki, kilichowakutanisha viongozi na wawakilishi wa vyama vya siasa na kusema kuwa lengo ni kujenga taifa la kidemokrasia na haki sawa kwa wote.

Alisema Dira 2050 imeyaweka mambo hayo kwa kuzingatia maoni ya wananchi hususani ya wawakilishi wa vyama vya siasa, waliyoyatoa Agosti 27, 2024.

"Tunataka Tanzania kuwa taifa la kidemokrasia, likiongozwa na katiba imara, inayoakisi muafaka wa kitaifa, taasisi madhubuti za umma na mfumo thabiti wa vyama vya siasa," alisema Prof. Mkumbo.

"Tunachokipendekeza kwenye dira ni kujenga picha kubwa ya tunataka taifa liweje. Tunataka tujenge taifa ambalo ni jumuishi, lenye ustawi, haki na linalojitegemea."

Kuhusu pato la nchi, alisema limekua mara nne kutoka Sh. trilioni 32 mwaka 2000 hadi Sh. trilioni 150, mwaka huu na kwamba makadirio ya sasa ya wachumi yanaonesha ukiwekwa msukumo mahsusi kwenye sekta 10, litafikia Sh. Trilioni 1.5 mwaka 2050.

Alisema wachumi wameeleza kuwa ikiwa makadirio yatakuwa ni kukua mara nne kama ilivyokuwa 2000/2025, Pato la Taifa litafikia Dola za Marekani bilioni 400 (karibu Sh. trilioni moja).

Alisema dira mpya inalenga kuondoa umasikini kwa kuhakikisha Tanzania inakuwa mzalishaji mkubwa wa chakula barani Afrika na kuwa miongoni mwa wazalishaji 10 duniani. Prof. Mkumbo alisema tayari wameshakubaliana ndani ya serikali kwamba mipango yote ya nchi ya muda mfupi, wa kati na mrefu, ijadiliwe na kuidhinishwa na Bunge.

"Kwa kuzingatia hilo, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, ameelekeza kwamba dira hii tofauti na dira iliyopita, lazima ikaidhinishwe bungeni. Inamaanisha kwamba itatungiwa sheria kwa hivyo kwa sababu hiyo, kutakuwa na legal protection (ulinzi wa kisheria), kwa maana ya kwamba yeyote atakayekuja huko mbele hawezi akasema atakuwa na dira yake nyingine, itakuwa ni hii hii itabidi aisimamie," alisema.

Mbali ya hilo, alisema rasimu ya Dira 2050 ina maeneo makubwa matano ambayo ni Msingi Mkuu uliojikita kwenye utawala, amani, usalama na utulivu.

Prof. Mkumbo alisema itasimamiwa na nguzo tatu ambazo ni uchumi imara na jumuishi, uwezo wa watu na maendeleo ya jamii, uhifadhi wa mazingira na uhimilivu wa mabadiliko ya tabia nchi.

Alisema Dira 2050 imetaja pia miundombinu fungamanishi ambayo itahusisha barabara, reli na usafiri wa majini, sayansi na teknolojia, utafiti na maendeleo, mageuzi ya kidijitali na nishati.

Alisema imeweka sekta 10 za kimageuzi ambazo ni kilimo, huduma za watumiaji, utalii, madini, uzalishaji viwandani, huduma za fedha, ujenzi, uchumi wa buluu, michezo na sanaa za ubunifu, zitakazowekewa mkazo mahsusi.

Alisema huduma za kijamii kama elimu, afya, hifadhi ya jamii, umiliki wa ardhi, maji na ustahamilivu wa mabadiliko ya tabia nchi, nazo zitapewa uzito mkubwa.

"Ardhi yote ya Tanzania kupangwa na kupimwa kwa matumizi mbalimbali. Ardhi kwa ajili ya makazi bora, kilimo, mifugo na uwekezaji," alifafanua.

Wakitoa maoni, Makamu Mwenyekiti wa Chama cha ACT Wazalendo, Isihaka Mchinjita, alisema rasimu hiyo inahitaji maboresho kwenye muundo wa uchumi kwa kuweka mkakati wa kuongeza thamani mazao ya kilimo na malighafi zote zinazopatikana nchini. Pia alitaka Watanzania wote wenye umri wa miaka 18 waingizwe kwenye hifadhi ya jamii. Naye mwakilishi wa TADEA, Ali Makame Issa, alishauri ardhi yote ipangiwe matumizi, ili kulinda inayotengwa kwa shughuli za kilimo. Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, aliishauri tume isifunge milango ya kupokea maoni yakiwamo ya maandishi.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***



Mafundi wa Shirika la Umeme Tanesco, wakichimba mashimo kwa ajili ya kusimika nguzo za kufunga waya za nishati hiyo katika eneo la Mikocheni Dar es Salaam jana.
**PICHA: JUMANNE JUMA**

# Siri Wachaga kurudi kwao mwisho wa mwaka

**Na Waandishi Wetu, MOSHI**

MOJA ya swali unaloanza kujiuliza inapofika kila mwisho wa mwaka ni siri gani iliyojificha kwa kabila la Wachaga kuiteka nchi kwa shamrashamra zinazotokana na utamaduni wa kurudi kwao kuhiji wakiwa makumi kwa maelfu.

Watu wengi wanafikiria kwamba Wachaga wanatokana na asili moja. Ukweli ni kwamba wamegawanyika katika himaya 15, wanatofautiana kwa lafudhi, lugha, rangi na mwonekano wa miili yao.

Utamaduni wa Wachaga wa kufunga safari kila mwaka kurudi nyumbani msimu wa krismasi, umekuwa ukiwashangaza wengi na kuwaacha na maswali yasiyo na majibu.

Mzee Jossen Abel Moshi (87), Mkazi wa Mbokomu, Moshi mkoani Kilimanjaro, anasema utamaduni huo unajengwa na hoja kwamba huwa wanarejea makwao kila mwisho wa mwaka kwa ajili ya kupumzika na kujadili mambo yao.

"Wanakuja kupumzika baada ya kufanya kazi zao kuanzia Januari mpaka Desemba, wanarudi nyumbani kuungana na wenzao na hata wengine ambao hujawahi kuwaona kwa kipindi cha mwaka mzima, basi wanakuja nyumbani kusherehekea hiyo sikukuu na kupumzika," anasema.

Alipoulizwa kama kweli wanakwenda kufanya matambiko. Mzee Moshi anasema: "Yale mambo ya kizamani ya kufanya matambiko yalishaisha kabisa; na kipindi kile watu walikuwa hawasafiri sana, walikuwa wanaishi tu nyumbani, wala hawakuwa wanatoka mbali.

"Isipokuwa mwisho wa mwaka, huwa wanakuja nyumbani wanachinja mbuzi, ng'ombe kwa ajili ya kusherehekea krismasi na mwaka mpya, kulingana na jinsi familia au ukoo wao walivyo wengi. Hili linategemea na uchumi wa kila familia au koo.

"Wanapokutana kula hicho chakula, huwa wanakutana kuongea mambo yao ya kifamilia, kukemea uvivu, ulevi na hata kusaidiana ndugu wanapokwama kiuchumi. Kimsingi huwa wanakemeana kwa wale wanaoonekana wanaenda kinyume na malengo ya familia.

Watoto wa kiume, walevi, kinababa wavivu, hivyo vikao kwao huwa ni vigumu kwa sababu wanakemewa mpaka na watoto wao, kwa kuwa mambo hayo yanaweza kusababisha hata njaa kwenye familia na uchumi wao kuyumba." Kiongozi wa mila ya Kichaga kutoka Rombo Mshili, George Kavishe, alisema dhana kwamba Wachaga hurudi nyumbani mwisho wa mwaka kufanya matambiko, sio sahihi.

Alisema wanachorudi kukifanya, ni kuienzi mila iliyo njema ya kukutana na wapendwa wao, baada ya muda mrefu wa utafutaji.

"Katika kukutana na wapendwa wao, yapo mambo mengi yanayofanyika, ikiwemo kufanya ibada za familia, kufanya usafi kwenye makaburi, kutatua migogoro ikiwa ipo, na hii ni ishara njema ya umoja na upendo.

"Usimamizi huo unaleta tija katika koo husika zipo nyakati wanapendekeza mambo ya kimaendeleo, ikiwemo kuoa, kuacha tabia zilizo mbaya miongoni mwa jamii na kuongeza ushirikiano," alisema.

Mchili wa Wachaga wa Mwika, Laurence Mlay, zaidi alifafanua akisema: "Wako wachache kwenye jamii, ambao wanakaidi kutokana na tabia hizo kuota mizizi, ila tunahakikisha tumewachukulia hatua kwa kushirikiana na serikali.

"Wale wote wanaoshindwa kuja nyakati za sikukuu za mwisho wa mwaka, sisi tunawahesabu kama wavivu na wasiojituma hivyo serikali iwachukulie hatua."

Mangi wa Machame, Gilbert Shangali, alisema yeye kama kiongozi wa mila, hatavumilia wavivu na wanywaji wa pombe kupitiliza katika jamii ya kabila 52.

"Nitashirikiana na serikali katika kuleta mabadiliko chanya kwa jamii, nitapinga uvivu, wizi, matumizi ya madawa ya kulevya, ukatili na utelekezaji wa watoto, wanawake na wazee,"alisema Mangi Shangali.

**•Imeandikwa na Godfrey Mushi na Mary Mosha (Moshi).**

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

HABARI KITAIFA

## Ajali yaua wanne, watatu wajeruhiwa

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

WATU wanne wamefariki dunia papo hapo na wengine watatu kujeruhiwa baada ya gari walilokuwa wakisafiria kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza, kugongana uso kwa uso na lori la mizigo.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) Hamis Mungwana, alisema tukio hilo lilitokea jana asubuhi katika Kijiji cha Unyampiti, Kata ya Unyahati, wilayani Ikungi, mkoani Singida.

Alisema ajali hiyo imehusisha gari aina ya Toyota Alphard lenye namba za usajili T 128 EKF, mali ya Anastazia Gozbert, ambayo iligongana na lori lenye namba za usajiri T 467 EJP ikiwa na tela lake, T 439 EJN aina ya Howo, mali ya East Africa Logistic Ltd, ambayo lilikuwa likitokea Singida kwenda Dar es Salaam.

Mungwana alisema waliofariki dunia ni wanaume na majina yao hayajafahamika na miili yao imehifadhiwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Singida (Mandewa).

Alisema kati ya majeruhi watatu, mmoja ametambuliwa ambaye ni Mauldi Mbalima, mfanyabiashara wa Korogwe Pwani ambaye amejeruhiwa miguu.

"Majeruhi wengine wawili wanaokadiriwa kuwa na umri wa miaka 30 hadi 45 hali zao ni mbaya na wanaendelea na matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Singida," alisema.

Kamanda Mungwana alisema chanzo cha ajali hiyo ni dereva wa gari aina ya Toyota Alphard kuendesha gari kwa kasi na kwenda upande wa pili na kugonga lori la mizigo.




Mafundi wa Mtandao wa Mawasiliano, wakifanya matengenezo ya kuimarisha mawasiliano katika eneo la Kitunda jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Bei za vyakula hazishikiki sokoni

**Na Waandishi Wetu**

ZIKIBAKI siku 11 kabla ya Sikukuu ya Krismasi, bei za vyakula na bidhaa zimeendelea kupaa katika masoko maeneo mbalimbali nchini.

Uchunguzi uliofanywa na Nipashe, umebaini kuwa kilo moja ya maharage kwa sasa imepanda hadi Sh. 4,000 wakati awali iliuzwa Sh. 3,500 na nyama ya ng'ombe kilo imefikia Sh. 12,000 wakati awali iliuzwa kati ya Sh. 9,000 hadi Sh. 10,000 kulingana na eneo husika.

Kuku wa kisasa ambaye alikuwa akiuzwa Sh. 8,000 amefikia Sh. 11,000 na wale wa kienyeji wanauzwa hadi Sh. 30,000 wakati bei ya awali ilikuwa Sh. 20,000 hadi Sh. 25,000.

**MIKOA YA KASKAZINI**

Katika miji ya Bomang'ombe na Machame, baadhi ya maeneo ya Sanya Juu, Moshi Mjini (Kilimanjaro) na Arusha Mjini, kilo moja ya nyama ya ng'ombe inauzwa Sh. 12,000 kwa sasa wakati awali ilikuwa Sh. 10,000.

Akizungumza na Nipashe, Joseph Laitayo, mfanyabiashara wa nyama katika mji wa Bomang'ombe, wilayani Hai, alisema nyama ya ng'ombe imepanda tangu Septemba, mwaka huu, kutokana na kupanda kwa bei ya ng'ombe mnadani.

Alisema nyama ya steki ambayo huuzwa tofauti na mchanganyiko wa nyama wa kawaida, inauzwa kwa Sh. 14, 000 kwa kilo katika baadhi ya maeneo kwenye wilaya za Hai, Moshi na Arusha.

Wakati mbuzi mmoja wa 'ndafu' ambayo ni maarufu kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kifamilia, bei ya mnadani ni kati ya Sh. 250,000 hadi 300,000 kulingana na ukubwa wa mbuzi. Wananchi mkoani Manyara, wamesema bei za vyakula muhimu, haitishi kwa kuwa bado havijapanda.

Mkazi wa Mtaa wa Komoto, Edina Charles, alisema kwa sasa wananunua kilo moja ya sukari Sh .2, 700 huku bei ya mchele ikiwa ni Sh. 2,000 mpaka Sh.2,800 kwa kilo.

Muuzaji wa vyakula vya nafaka, Ally Hamis, alisema maeneo mengi mchele unakolimwa kwa sasa wakulima ndio wanapanda, hivyo kusababisha upatikanaji wake kupungua

**SINGIDA**

Katika soko kuu la Singida, Ginery, Misufini, Kibaoni, Mahambe, Minga na soko la Unyankindi, bei za vyakula zimeongezeka, hivyo kuzua malalamiko kwa wananchi na wafanyabiashara wenyewe.

Vyakula vilivyopanda bei ni pamoja na viazi mviringo ambavyo vilikuwa vinauzwa kwa Sh. 90,000 kwa gunia la ujazo wa kilo 100 lakini hivi sasa linauzwa kati ya Sh. 105,000 na Sh. 110,000.

Mkungu mmoja wa ndizi (ndizi Bukoba) ambao ulikuwa unauzwa kati ya Sh. 25,000 na 27,000 hivi sasa unapatikana kwa Sh. 33,000 hadi 35,000.

Maharage ya njano ambayo yalikuwa yanauzwa kwa Sh. 2,500 hadi 3,000 kwa kilo lakini hivi sasa katika masoko hayo, yanauzwa kwa Sh. 3,500 hadi 4,000 kwa kilo huku mchele supa kwa kilo unauzwa Sh. 4,000 kutoka Sh.3,500.

Kuhusu matunda, bei ya embe ya jumla ilikuwa ikiuzwa kwa Sh. 200 lakini sasa inauzwa kwa Sh.350 wakati limau moja linauzwa kwa Sh. 500 hadi Sh. 700.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wananchi na wafanyabiashara katika masoko hayo, walisema bei hizo za vyakula zilianza kupanda baada ya msimu wa masika kuanza.

Mwenyekiti wa Soko Kuu la Singida, Hassan Mboroo, alisema wafanyabiashara wanaoleta vyakula katika masoko wamepandisha bei za vyakula wakidai ni kutokana na changamoto ya usafiri iliyosababishwa na mvua nyingi kunyesha na kuharibu miundombinu.

Mfanyabiashara wa ndizi, Robert Kiato, alisema bei hizo za vyakula zinaweza kupanda zaidi kadri mvua zinavyoendelea kunyesha, huku changamoto ya kusafirisha vyakula kwenda kwenye masoko ikizidi kuwa kubwa.

**DODOMA MOTO**

Katika soko kuu la Majengo jijini Dododma, bei ya kilo ya nyama imepanda kutoka Sh. 8,000 mwezi uliopita hadi kufikia Sh. 11,000 kwa sasa na kilo ya mchele ambayo ilikuwa Sh. 1,600 kwa sasa inauzwa Sh. 3,000.

Bidhaa zingine zilizopanda ni unga wa sembe kutoka Sh. 1,000 kwa kilo hadi kufikia 1,500, maharage kilo ni Sh. 3,600 kutoka Sh. 3,000 na mafuta ya kupikia lita moja Sh. 5,000 kutoka Sh. 4,500.

Bei ya samaki aina ya sato imepanda ambapo kilo moja imefikia Sh. 14,000 kutoka Sh. 12,000 huku samaki aina ya sangara aliyekuwa akiuzwa Sh. 10,000 kwa sasa ni Sh. 12,000.

Salum Abubakar alisema hali ya bei ya vyakula jijini humo hivi sasa imeendelea kupanda na kuzitaka mamlaka husika kuingilia kati kudhibiti hali hiyo.

Alisema hali hiyo isipoangaliwa mapema inaweza kuwa mbaya zaidi hasa itakapofikia mwezi Januari na Februari wakati mvua za masika zitakapokuwa zimekolea.

Akizungumza na gazeti hili muuza bucha la nyama eneo la Kikuyu Hassan Maliseli, alisema sababu za kupanda kwa bei hiyo kunatokana na upatikanaji adimu wa ng'ombe katika baadhi ya machinjio, lakini pia inahusisha kupanda huko na msimu wa sikikuu.

Nipashe imeshuhudia katika soko la majengo, Dodoma, sado moja linauzwa Sh. 7,000 badala ya Sh. 3,500, huku ndoo ya lita 20 vinauzwa Sh. 22,000 badala ya Sh. 18,000 ya awali.

Muuzaji wa vitunguu sokoni hapo, Aisha Selemani, alisema upatikanaji wa bidhaa hiyo kutoka kwa wakulima umekuwa changamoto, hali inayochangia bei kuongezeka.

Erick Moses, muuzaji wa mayai ya jumla, alisema trei mayai imepanda kutoka Sh. 8000 kwa bei ya jumla mpaka Sh. 10,000 na kwa wauzaji wa rejareja inauzwa Sh. 12,000, huku yai moja likiuzwa Sh. 400 badala ya Sh. 300.

Alisema kupanda kwa bei ya mayai kunatokana na msimu wa sikukuu lakini pia, walanguzi wa bidhaa hiyo wamekuwa wengi na kusababisha wafugaji kushindwa kumudu soko la wateja.

**HALI DAR ES SALAAM**

Mfanyabiashara wa mchele na maharage kwa bei ya jumla katika Soko la Tandale, Kassim Said, alisema mwezi Novemba na Desemba, bei za mazao hayo hupanda kwa sababu wakulima huyaficha wakisubiri msimu wa mvua uanze.

Alisema maharage yanayotoka mkoani Tanga wanauziwa na wakulima kwa Sh. 2,900 kwa kilo na wao huuza Sh. 3,300 na yakifika madukani yanauzwa Sh. 3,800.

Mfanyabiashara wa nyanya kwa bei ya jumla Soko la Mabibo , Ramadhani Seif, alisema walilazimika kupandisha bei ya matenga ya nyanya kutoka Sh.35,000 hadi Sh.50,000 kwa sababu wakulima wanawauzia Sh.25,000 hadi Sh. 35,000, kulingana na ubora wa nyanya zilizoko kwenye tenga.

Mfanyabiashara wa vitunguu katika soko la Mabibo, Charles Michael, alisema kwa sasa wananunua gunia la vitunguu kwa wakulima wa mkoani Njombe, kwa Sh. 100,000 kutoka Sh. 50,000, hivyo kulazimika kuuza bei ya jumla ya Sh. 180,000 kutoka Sh. 100,000.

Amina Juma, mkazi wa Sinza, alisema kwa sasa kitunguu kimoja kinauzwa kati ya Sh. 500 hadi 600.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# Wenye uvimbe kwenye uzazi wasimulia mateso kila mwezi

**Na Jenifer Gilla**



Waziri wa Afya, Jenista Mhagama. **PICHA:MTANDAO**

Ni simulizi ngumu zilizojaa mateso kwa wanawake wenye tatizo la uvimbe kwenye kizazi (fibroids), wapo ambao wamefanyiwa upasuaji zaidi ya mara tatu lakini tatizo limerejea upya na wengine huishia kuwa wagumba.

Wanasimulia nyakati ngumu za maumivu makali wanazokutana nazo kila mwezi wakati wa hedhi, kupoteza damu nyingi na namna tatizo hilo linavyohatarisha ndoa zao na hali zao za kiuchumi.

Mkalimani wa lugha, Happy Dismas (33), mkazi wa Chang'ombe, Temeke mkoani Dar es Salaam ambaye hajajaliwa kupata mtoto hadi sasa, anasimulia namna anavyoshindwa kwenda ofisini wakati mwingine hadi siku nne kila mwezi kutokana na kutokwa damu nyingi wakati wa hedhi ikiambatana na maumivu makali.

Mwanamke huyu ambaye ni mwajiriwa katika ofisi binafsi, anasimulia kwamba, hali hiyo wakati mwingine inamletea shida kwa bosi wake.

Anasema kwa nafasi yake, asipohudhuria ofisini husababisha kuwapo mrundikano wa kazi na kusababisha baadhi ya huduma kusimama.

"Katika kitengo changu nipo mwenyewe kwa hiyo nisipokuwapo, kazi zinasimama. Wakati mwingine nikiwa ninapitia hali hii, ninalazimika kufanya kazi za ofisini nikiwa nyumbani, ili tu nisimkwaze bosi wangu," anasimulia.

Happy anasema hali hiyo huchangia kuishiwa damu, kukosa raha na huwa kwenye msongo wa mawazo kwa sababu licha ya miaka minne nyuma kufanyiwa operesheni na kuondolewa uvimbe huo, umerejea tena.

"Daktari alinieleza ili kumaliza tatizo hili kabisa ninatakiwa kufanyiwa operesheni ya kuondolewa kizazi, jambo ambalo kwa kweli sikubaliani nalo kwa sababu ninahitaji kuzaa," anasema.

Mfanyakazi wa benki, Luciana Kavishe (40), mkazi wa Mbezi, Dar es Salaam, anaweka wazi kwamba, tatizo hilo la uvimbe kwenye uzazi lilimsababishia kutoifurahia ndoa yake kwa miaka mitatu kutokana na kila alipopata ujauzito uliharibika.

Anasema kutokana na hali hiyo, mwaka jana baada ya kushika ujauzito wa tano alilazimika kwenda hospitalini kufanyiwa huduma ya kushonwa kizazi na kupewa huduma ya mapumziko (bedrest) hadi pale mimba ilipokomaa na kufanyiwa operesheni.

Luciana anasema tofauti na wengine ambao wanapojifungua kwa operesheni hutolewa na uvimbe, kwake ilishindikana na madaktari walimweleza sababu ni kwamba, uvimbe aliokuwa nao ulikuwa mkubwa, hivyo ungechangia kutokwa damu nyingi.

"Bado nina uvimbe mkubwa. Ninapitia changamoto kwa sababu ninalea mtoto mdogo huku nikipitia maumivu makali ya uvimbe. Ninalazimika kila siku kunywa dawa za kupunguza maumivu. Ninasubiri mtoto akue kidogo ili niende kuutoa," anasimulia Luciana.

Simulizi hizo na madhila waliyopitia watangulizi haitofautiani na ya Maria Khamisi (45) mkazi wa Ilala, Dar es Salaam, aliyeishi na uvimbe wa namna hiyo kwa miaka 10, ingawa yeye anasema ilimchukua muda huo kutokana na kukosa fedha za matibabu.

Anasema alifanyiwa upasuaji na kutolewa uvimbe mwaka jana, baada ya ndugu zake kumchangia fedha kutokana na hali yake kuwa mbaya zaidi.

"Shida niliyopitia kwa miaka yote 10 ilipopatikana fedha ili nifanyiwe upasuaji niliwaambia madaktari watoe kizazi kwani sikutaka tena kupitia maumivu makali wala changamoto nilizopitia," anasimulia.

Wakati simulizi hizo zikitolewa, ripoti ya Taasisi ya National Library Medicine (2024) inaonesha karibu asilimia 80 ya wanawake weusi kutoka nchi za Jangwa la Sahara wanapatwa na tatizo hilo na kusababisha changamoto kadhaa ikiwamo kukosa uwezo wa kubeba mimba.

**KITAALAMU**

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Kinamama na Masuala ya Uzazi Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Lilian Mnabwiru, anasema uvimbe unaojitokeza kwenye mfumo wa uzazi usipotibiwa mapema unaweza kuleta madhara makubwa kama vile kupungukiwa damu na ugumba.

Anasema uvimbe huo unaweza kutokea katika ngozi ya nje ya uzazi, misuli katikati au katika ngozi laini ya tumbo la uzazi la ndani anapokaa mtoto au katika mlango wa uzazi.

Anasema mara nyingi mwanamke anaweza kupata tatizo hilo anapokuwa katika umri wa uzazi wa miaka 18-40 kwa sababu ni kipindi ambacho mwili hutengeneza homoni za kike kwa wingi.

"Uvimbe huu husaidiwa kukua zaidi na homoni zijulikanazo kama Estrogen na Progesterone hasa katika umri wa uzazi. Mara nyingi hutokea katika familia yenye historia ya matatizo hayo na imegundulika kuwa wanawake wengi weusi wanapata sana hili tatizo" anafafanua mtaalamu huyo.

Anasema si rahisi kwa mwanamke mwenye tatizo hilo kujigundua mapema kwa sababu huwa hautoi dalili za moja kwa moja kama bado haujafikia saizi kubwa.

"Mwanamke anaweza kujiona amenenepa au anapata kitambi, kumbe uvimbe unakua taratibu kwa sababu unapokuwa upo katika saizi ndogo huwa hauleti madhara yoyote.

"Dalili ni maumivu ya tumbo la chini, kupata shida wakati wa kupata haja ndogo, kupata hedhi kwa muda mrefu na nyingi. Mtu anaweza kutumia hata pakiti mbili za pedi. Kutoshika mimba na huchangia upungufu mkubwa wa damu mwilini," anasema.

Mtaalam huyo anasema mwanamke anaweza asipate ujauzito iwapo uvimbe utakuwa katika mlango wa kizazi ambapo huzuia mbegu za kiume zisiingie au endapo katika milango ya mirija kwa ndani itazuia utungaji wa mimba.

Kuhusu matibabu, Dk. Mnabwiru anasema yanategemea na umri wa mgonjwa na kama atakuwa anahitaji mtoto au laa au hutegemea ameathirika kwa kiwango gani.

"Mara nyingi uvimbe wenyewe ukiwa mdogo kuanzia sentimia moja au mbili huwa hauleti shida lakini kuanzia sentimita nne, tano, sita, saba inabidi kufanya matibabu kama itakuwa sentimita tatu ipo ndani ya mji wa mimba matibabu yake pia yapo.

"Kwa wale ambao hawana dalili kubwa, kuna matibabu mbadala. Kuna mfumo ambao tunautumia tunakwenda kutibu mishipa mikubwa inayosambaza damu kwenye kizazi na hivyo kufanya uvimbe usinyae," anasema.

Matibabu mengine anayataja mtaalam huyo ni yanayohusisha mionzi maalum ya 'ultrasound' na pia, dawa za sindano au vidonge anahamasisha wanawake kujenga utamaduni wa kupima afya zao mara kwa mara kwa sababu dalili zake hazionekani mapema, huku akibainisha kwamba, asilimia kubwa ya wanaowagundua huwa hawajui kama wana uvimbe.

Anasema kwa siku wana kliniki ya wagonjwa 100 ambapo kati yao, hawakosekani wanawake 30 wenye tatizo hilo.

Daktari wa Afya katika Hospitali ya Aga Khan, Gregory Ntiyakunze, anasema zipo njia mbalimbali za kumtibu mgonjwa wa aina hiyo, lakini kwa yule anayetokwa na damu nyingi na hapendi kufanyiwa upasuaji, hupatiwa dawa za kuzuia hedhi kwa muda fulani, ili kumsaidia asipungukiwe damu anapokuwa katika hedhi.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake na Kizazi Hospitali Sant Francis Morogoro Dk. Elius Kweyamba, anasema asilimia 40 hadi 60 ya wanawake, wanaishi na uvimbe huo bila kujua na hawaoni athari yoyote.

Anasema katika kliniki yao mgonjwa umri mdogo waliyewahi kumwona ni mwenye umri wa miaka 25.

Dk. Kweyamba anasema operesheni kwa mgonjwa hutegemea na hali ya tatizo la mgonjwa na huweza kufanyiwa hata zaidi ya mara tatu.

"Wagonjwa ninaokutana nao katika kliniki yetu, kati ya 20 ninaowaona kwa siku, wenye tatizo huwa kati ya watu watatu hadi watano ikiwa ni asilimia 80 karibu ya kina mama wote wanaishi na tatizo hilo," anasema.

**MADHARA AFYA AKILI**

Mwanasaikolojiatiba kutoka Kituo cha Afya cha Somedics Polyclinic, Saldeen Kimangale, anasema wanawake wengi wanaougua ugonjwa huo, wanapitia tatizo la afya ya akili, kwa sababu huwaathiri katika nyanja mbalimbali na kudumaza uwezo wao wa kukua kijamii.

Anasema hukabiliwa na mabadiliko makubwa na ya mara kwa mara na wakati mwingine ya ghafla yanayohusiana na kihisia, huzuni, hasira, tafrani, uchungu na maumivu.

Kimangale anasema husababisha kushindwa kutekeleza majukumu yao ya kila siku ikiwamo uzalishaji mali, jambo linalodhoofisha ubora wa maisha yake.

"Gharama kubwa za matibabu na hofu ya kutokuwa na suluhisho la haraka, huongeza msongo wa mawazo na hivyo kuzidisha changamoto katika afya yake ya akili na ustawi wake wa kisaikolojia," anasema.

Anakiri kwamba hupokea wagonjwa wa aina hii wanaohitaji tiba ya kisaikolojia ambapo huwapatia huduma ya kuwaimarisha kimtazamo na kihisia.

Kadhalika huwapatia tiba ya kuwaongoza wawe na uwezo wa kukabiliana na jambo moja baada ya jingine, kuwasaidia kutenganisha ugonjwa na wao binafsi.

"Katika tiba hizi tunawaongoza kutambua kuwa ugonjwa usiwe ndio tafsiri ya utu wao. Tunawasaidia kuwa na mtindo mzuri wa maisha utakaowapunguzia adha ya ugonjwa kwa sababu baadhi ya tabia huchochea tatizo au kulikuza.

"Lakini pia inapobidi tunahusisha familia ili waweze kumpatia msaada sahihi na kwa wakati hasa nyakati ambazo hisia zake zinakuwa zinabadilika," anasema.

Mtaalam huyo anasema huwafundisha mbinu mbalimbali za kujipatia utulivu na kukabiliana na msongo wa mawazo na huwapa matumaini ya kushinda changamoto zinazotokana na uvimbe kwenye kizazi.

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*

HABARI KITAIFA

# Watoto wanne wafa maji kwa kuzama kwenye dimbwi

**Na Remmy Moka,**
MWANZA

WATOTO wanne wamefariki dunia katika Kijiji cha Isemvya, kata ya Lagangabilili, wilaya ya Itilima, mkoani Simiyu, baada ya kuzama kwenye dimbwi lililochimbwa katika makazi ya watu kwa ajili ya madini.

Imeelezwa kuwa, walikwenda hapo kwa ajili ya kufua na kuchota maji kwa matumizi ya nyumbani.

Kati ya watoto hao, wawili ni wa familia mmoja na miongoni mwao, watatu ni wanafunzi katika Shule ya Sekondari Lagangabilili.

Mmoja wa wazazi wa watoto hao, Justine Kibunje, alisema baada ya kupokea taarifa ya watoto hao kuzama, alikwenda kujaribu kuwaokoa, lakini kutokana na hali ya mshtuko, naye akanusurika kuzama katika dimbwi hilo.

"Ile hofu na mshtuko niliokuwa nao nilikimbia kuingia katika maji, nikazidiwa na sikuweza kufanya lolote," alisimulia mzazi huyo.

Mzazi mwingine, Happyness Mbise, alisema amepoteza nguvu kazi ya familia na taifa kwa ujumla, kwa sababu mtoto wake alikuwa ndio tegemeo lake.

Baadhi ya wakazi wa maeneo hayo akiwamo Salum Gola, waliiomba serikali kufanya jitihada madhubuti kuhakikisha mashimo hayo yanafukiwa, ili kuweka hali ya usalama katika maeneo ya makazi.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Simiyu, (ASF) Faustine Mtitu, alithibitisha kuopolewa kwa miili hiyo minne, kwa kushirikiana na wananchi.

Aliwataja watoto hao ni Neema Masung (16), Mary Kibunje (17), Nkwaya Justine (15) na Lusia Samson (16).

Mtitu alisema matukio ya ajali za namna hiyo yanaongoza mkoani humo kwa kusababisha vifo, hivyo kuwataka wananchi kuchukua jitihada za makusudi, ikiwa ni pamoja na kufukia mashimo yote yaliyoko katika makazi yao, kwani kuendelea kubaki hivyo kutasababisha madhara ya namna hiyo.

Katika hatua nyingine, zaidi ya wanafunzi 10 waliokuwa wakisoma masoma ya ziada katika Shule ya Msingi Bariadi Alliance, wilayani Bariadi, mkoani Simiyu, wamenusurika kifo baada ya bweni kuungua, huku chanzo chake bado hakijafahamika.

Mkurugenzi wa Shule hiyo, Jackson Yuma, alisema madhara yanayotokana na moto huo ni kuungua kwa baadhi ya vifaa vya wanafunzi yakiwamo magodoro na kwamba, hakuna athari ya kibinadamu.



Baadhi ya waajiri kutoka sekta binafsi mkoa wa Ubungo jijini Dar es Salaam wakimsikiliza Meneja wa NSSF wa mkoa huo, CPA Joseph Fungo wakati akifungua semina kuhusu wajibu wa waajiri kusajili na kuwasilisha michango ya wanachama wao mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## NSSF yawanoa waajiri wa sekta binafsi

**Na Mwandishi Wetu**

MFUKO wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), umetoa mafunzo kwa waajiri wa sekta binafsi wanaohudumiwa na ofisi ya mfuko huo, Mkoa wa Ubungo, Dar es Salaam.

Mafunzo hayo yamefanyika mwishoni mwa wiki katika ofisi zao za Ubungo, yakiwa na lengo la kuwakumbusha waajiri majukumu yao yakiwamo, kusajili wafanyakazi wao na kuwasilisha michango kwa wakati, kwani hilo ni takwa la kisheria.

Mada mbalimbali zilizotolewa katika mafunzo hayo ni matakwa ya Sheria ya Mfuko na Matumizi ya Mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHEMA) iliyoboreshwa (Employer Portal).

Ofisi ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Wilaya ya Ubungo, ziliwasilishwa na Devotha Mihayo, ambaye ni Mkuu wa ofisi hiyo.

Akifungua semina hiyo, Meneja wa NSSF, Mkoa wa Ubungo, CPA. Joseph Fungo amewashukuru waajiri wa sekta binafsi kwa kushiriki mafunzo hayo yenye lengo la kutoa elimu ya hifadhi ya jamii kwa waajiri.

Kadhalika alisema mafunzo hayo yanalenga kuwakumbusha waajiri kutimiza wajibu wao kwa mujibu wa sheria ikiwa ni pamoja kutoa taarifa za wafanyakazi wasiosajiliwa ili mfuko uweze kuwasajili na kisha kuwasilisha michango kwa wakati

Fungo alisema suala la kutoa elimu kwa wanachama na waajiri wa sekta binafsi wa mkoa huo litaimarisha ushirikiano kwa waajiri na NSSF na kuongeza mafanikio ya utoaji wa huduma bora kwa wanachama na wadau kwa ujumla.

Geofrey Ngwembe, Ofisa Sheria wa NSSF, alitumia mafunzo hayo kuwakumbusha waajiri hao kutekeleza wajibu wao kisheria katika kuhakikisha michango ya wanachama inawasilishwa kwa wakati pamoja na kuwajengea uelewa kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu sheria ya hifadhi ya jamii.

# Madini ya vito kuuzwa kielektroniki kuongeza uwazi




**Na Cynthia Mwilolezi,**
SIMANJIRO

WAZIRI wa Madini, Anthony Mavunde, amezindua mnada wa ndani wa madini ya vito ya gramu 184.06 yenye thamani ya Sh. bilioni 3.1, ambao umeendeshwa kwa njia ya kielektroniki ili kuongeza uwazi na ushindani.

Amesema pia, serikali inafanya utaratibu wa kuwarejeshea wafanyabiashara madini yao ya vito yaliyochukuliwa kwenye mnada wa mwisho uliofanyika mwaka 2017 na kuhifadhiwa Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Mavunde alisema hayo jana wakati akizindua mnada wa madini hayo ya vito uliofanyika katika kituo cha Magufuli, kilichoko Mirerani, Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara.

Alisema wizara hiyo imejipanga kuweka Shilingi trilioni moja kwenye mfuko wa serikali mwaka huu wa fedha, ambapo kuanzia Julai Mosi, mwaka huu, hadi Desemba Mosi, mwaka huu, kiasi cha fedha kilichowekwa ni Sh. bilioni 434.

Mavunde alisema hadi mwishoni mwa mwezi huu, watakuwa wameshaweka Sh. bilioni 500. Alisisitiza kwamba, serikali itaendelea kuchukua hatua za makusudi kulinda madini ya Tanzanite, ili kurejesha hadhi yake kimataifa kupitia minada ya ndani na ya kimataifa.

"Tangu serikali ilipositisha mnada wa madini ya vito mwaka 2017 ili kufanya maboresho, sasa tumeanzisha mnada wa ndani na kabla ya mwisho wa mwezi huu, tutafanya mnada mwingine wa wachimbaji wadogo na wanunuzi wadogo," alisema.

Kuhusu urejeshwaji wa madini ya wafanyabiashara yaliyobaki kwenye mnada wa mwisho wa mwaka 2017 na kuchukuliwa na serikali, Waziri Mavunde alisema, kutafanyika tathmini ili wafanyabiashara wote ambao madini yao yalichukuliwa warejeshewe.

"Ninajua kuna hisia na dhana potofu kuwa serikali itachukua madini yatakayobaki katika mnada huu kama ilivyofanyika mwaka 2017.

"Ninataka niwahakikishie wafanyabiashara wote kwamba, madini yenu katika mnada huu yakibaki mtaondoka nayo, hakuna mtu atakayeyachukua," aliwahakikishia.

Kuhusu changamoto zilizowasilishwa na Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka, inayohusu zahanati kwenye eneo la migodi na ubovu wa barabara, Waziri Mavunde alisema, eneo limeshapatikana na serikali itapeleka fedha ili kuijenga.

"Tunatoa kipaumbele katika maeneo ya uzalishaji wa madini, hivyo ninataka niwahakikishie kwamba, tunaendelea kuwasiliana na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) ili barabara za ndani ya ukuta zifanyiwe ukarabati kwa haraka," aliahidi.

Kuhusu kero ya foleni ndefu ya ukaguzi wakati wa kutoka ndani ya ukuta ambayo wakati mwingine inafika hadi usiku wa manane, Waziri Mavunde alimwagiza Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, kuishughulikia mara moja.

Awali, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini, Msafiri Ndimbo, alisema mnada huo umejumuisha wanunuzi 195.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uchaguzi CHADEMA uimarishe demokrasia badala ya kuwagawa

**VUGUVUGU** la uchaguzi ndani ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) limepamba moto baada ya wiki hii, mwanasheria, mwanaharakati na mwanasiasa machachari, Tundu Lissu kutangaza kuwania nafasi ya mwenyekiti wa taifa wa chama hicho.

Uamuzi wa Lissu kugombea nafasi hiyo ambayo kwa sasa inashikiliwa na Freeman Mbowe kwa miaka kadhaa, imeamsha tashwishwi na hisia mbalimbali miongoni mwa wadau wa siasa. Baadhi ya wachambuzi wanasema huenda huo ukawa mwisho wa enzi wa kisiasa wa Mbowe ambaye ni mmoja wa waanzilishi wa chama hicho, wakiwamo kina Mzee Edwin Mtei na marehemu Bob Makani. Pia wanalitazama jambo hili kwa mtazamo wa mbali zaidi kwamba huenda huo ni mwisho wa CHADEMA baada ya kuwapo katika ulingo wa siasa kwa takriban miaka 22.

Huku akionekana kuungwa mkono na wafuasi wengi ndani ya chama hicho, Lissu alisema amedhamiria kugombea nafasi hiyo kwa lengo la kuleta mtazamo na mwelekeo mpya kufuta makosa yaliyojitokeza katika miaka kadhaa ndani ya chama hicho.

Lissu ambaye aliwahi kuwa Mbunge wa Singida Mashariki na mgombea urais katika uchaguzi wa mwaka 2020 akichuana na aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Hayati John Magufuli, pia ameweka bayana kwamba lengo lake kubwa ni kuleta mwamko mpya wa kidemokrasia ndani ya chama na siasa za Tanzania kwa ujumla.

Kutokana na kujitokeza hadharani na kutangaza kugombea nafasi hiyo, Lissu ameonekana kuwa na ushawishi na kukubalika katika maeneo mengi ambayo chama hicho kikuu cha upinzani kimeweka ngome na kuwa tishio katika siasa za ushindani.

Kwa upande mwingine, hatua hiyo ya Lissu, kwa wahafidhina na wafuasi wa upande mwingine ,inaonekana kama kuchochea vurugu na mpasuko ndani ya chama. Kwa mantiki hiyo, watu wa kundi hilo wanadhani kwamba Lissu amechukua hatua hiyo kuibomoa CHADEMA na hata kuisambaratisha katika medani za siasa.

Suala la kuwapo kwa mvutano au upinzani ndani ya chama, kwa watu wanaojua kwa umakini masuala ya siasa, si uadui wala kuibua migawanyiko ndani ya chama bali kukuza demokrasia ndani ya chama husika na medani ya kisiasa kwa jumla.

Kuibuka kwa upinzani ndani ya chama baina ya viongozi na wafuasi si dhambi bali ni kukomaa kwa demokrasia. Ukweli ni kwamba katika siasa zinazofuata mfumo wa kidemokrasia, hakuna mtu mwenye hakimiliki ndani ya chama, hivyo wanachama na wafuasi wa CHADEMA wanapaswa kutambua kuwa hatua hiyo inaonesha kukua na kukomaa kwa demokrasia, utawala bora na utawala wa sheria kwa kuheshimu katiba.

Hakuna umangimeza wala usultani ndani ya vyama vya siasa kwa kuwa kama demokrasia inavyobainisha, hakuna budi kuwa na ukomo wa madaraka pindi mtu anapokuwa madarakani, kwa hiyo, ni lazima kuwe na utaratibu wa mtu kukaa madarakani kwa muda maalum na baada ya hapo kuwapisha wengine.


Wahenga wanasema hakuna kinachodumu isipokuwa mabadiliko.

Pamoja na ukweli huo, wanachama na wafuasi wa CHADEMA wanapaswa kutambua kuwa uchaguzi ni mchakato wa kufanya mabadiliko kutoka enzi moja kwenda nyingine, hivyo mambo yanayoendelea sasa kwa kuwapo kambi zinazopingana ni kukomaa kwa demokrasia na kuonesha maana halisi ya jina la chama hicho.

Aidha mchakato unaoendelea ndani ya chama hicho usiwe mwanzo wa mpasuko wa chama bali iwe sehemu ya kuwajenga wana-CHADEMA na kuwa na nguvu moja kwa ustawi wa demokrasia na maendeleo Tanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wanawake watumie turufu hii kuibuka na ushindi

Na Sabato Kasika

**USAWA** wa kijinsia ni moja ya mambo ambayo wanaharakati wa kutetea haki za wanawake wanayapigania ili idadi yao iwe sawa na ya wanaume katika ngazi mbalimbali za uongozi.

Hata hivyo, kumekuwapo na mtazamo kwamba hawapendani na wanabaguana kwa itikadi za vyama. Kama hilo lina ukweli ndani yake, wanaweza kukwama kufikia lengo la usawa wa kijinsia.

Njia nzuri inayoweza kuwavusha kutoka walipo hadi kufikia lengo wanalotaka, ni kuungana na bila kujali itikadi za vyama vyao, kwani hiyo ni turufu nzuri ya kupambana na wanaume.

Ni vyema wanawake wasikubali kugawanywa kwa itikadi za vyama bali watambue kuwa umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Utengano huo unaweza kuwafanya wakaendelea kubaki nyuma.

Wanawake huwa wanajiita kuwa ni 'jeshi kubwa' kwa sababu ni wengi, hivyo wangetumia wingi wao kuwania uongozi na kupigiana kura badala ya kuendelea kuwa wapigakura tu.

Ikumbukwe kuwa jitihada za kuelekea usawa wa kijinsia katika uongozi zimeanza kuonekana, baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kuchukua nchi, na anaendelea kuwainua wanawake katika uongozi.

Ninakubaliana na kaulimbiu ya wanawake kuwa 'uongozi si misuli, ni akili', busara na hekima. Kwa kuwa wanaamini hivyo, watumie kaulimbiu hiyo kwa kuunganisha nguvu zao ili washinde.

Jambo la muhimu ni kwamba wanawake wasikubali kubebwa katika kuwania uongozi, kwani kubebwa ndiko kunakozaa rushwa ya ngono pale mwanamke anapotafuta kuchaguliwa kuwa kiongozi.

Rushwa ya aina hiyo inadhalilisha utu wa mtu na inaua. Hivyo, njia nzuri ya ushindi wa wanawake dhidi ya mfumo dume unaosababisha wabaki nyuma katika uongozi ni kuunganisha nguvu zao.

Upendo wao usiwe wa kipindi fulani lakini wakati wa uchaguzi wanatengana kila mmoja anafuata itikadi ya chama chake. Iwapo mtindo huo utaendelea, wajue kuwa watazidi kukwamisha usawa kijinsia.

Pamoja na juhudi hizo za kutaka kufikia usawa kwenye nafasi mbalimbali za uongozi, nina angalizo kidogo, ambalo linaweza kuwasaidia kupiga hatua kwenda mbele kwa haraka zaidi.

Angalizo hili ni kwamba ni muhimu kuepuka kuongeza wingi wa wanawake katika nafasi za uongozi bila kuangalia uwezo wa kuongoza, hali inayoweza kusababisha wasimudu nafasi wanazotafuta.

Ni muhimu kupata wanawake wenye uwezo wa kuongoza na wenye ushawishi katika jamii, sio kutafuta idadi kubwa tu ambayo haina manufaa kwao na hata kwa taifa kwa ujumla.

Wanawake hawana budi kujipanga kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 ili kuibuka kwa kushinda nafasi nyingi, sio kuendelea kutegemea viti maalum.

Kwa sasa wanawake wanaweza kufanya kampeni zinazoambatana na warsha, makongamano na semina ili kujengeana uwezo, kwani hatua hiyo itasaidia kuwafanya watambue kuwa wana haki ya kuchaguliwa.

Ninaamini hatua hiyo itasaidia pia kuwafanya wasiogope mfumo dume, unaogawa majukumu katika jamii kulingana na jinsia na kusababisha waendelee kuwa watu wa kulea na kutunza familia na kazi za nyumbani.

Anasema wanawake wanatakiwa kutawala uwanja wa siasa, kwa kuwa ni wengi kuliko wanaume na kwamba wingi huo bila kubaguana kutokana na itikadi za vyama, unaweza kuleta usawa wa kijinsia.

Kutokana na wingi wao, wanawake wanatakiwa kutawala uwanja wa siasa kuliko wanaume, wingi huo bila kubaguana kwa itikadi za vyama, unaweza kuleta usawa wa kijinsia haraka.

# MAKALA

## FIKRA MBADALA

# Viongozi tumieni vibali vyenu kikamilifu



Pascal Mayalla

LEO naendelea na somo kuhusu kibali. Katika toleo lililopita, tuliangazia maana ya kibali, kazi ya kibali, sifa ya kibali endapo kitatumika kikamilifu au kisipotumika kuna madhara gani na ni nani anayetoa kibali.

Katika mwendelezo wa somo hili, tutaangalia ni namna gani utamjuaje mwenye kibali. Je, Julius Nyerere, Ali Hassan Mwinyi na Benjamin Mkapa walikuwa na vibali?

Kwa vile kibali hutoka kwa Mungu na humpa amtakaye au ampendaye, kitendo cha mtu yeyote kuwa kiongozi wa nchi, hicho ni kibali tosha lakini kujua ni kibali cha kufanya nini na ni kibali cha muda gani, ni Mungu mwenyewe hupanga na ndiye pekee hujua.

Kuna watu wengi wana vibali tofauti tofauti lakini hawajui kuwa wana vibali hivyo kwasababu hakuna yeyote aliyewaambia kuwa una kibali fulani. Hata katika uongozi, tuna viongozi wengi si viongozi wa wito, vipawa, karama wala uwezo. Hawana vipawa vya uongozi wala karama zozote, vipaji vya uongozi na uwezo wa uongozi lakini wanapata uongozi wa umma kwa kutumia 'jeuri ya pesa'.

Kuna watoto wengi wanazaliwa na vibali, wazazi wao hawana uwezo wa kuwabaini mapema, hivyo mwisho wa siku vibali vyao vinafutwa. Kuna watoto wanazaliwa na vipaji fulani bila wazazi wao kuwabaini na kuwaendeleza, hivyo vipaji hivyo vinakufa. Kuna watoto wanazaliwa na uwezo Kiislamu wanaitwa ma Sherifu lakini usipowabaini, uwezo wao unapotea.

Namna ya mtu wa kawaida kuwatambua wenye vibali, ni jinsi tu mambo yao yanavyowanyookea. Kwa jicho tu la kawaida wanaonekana ni watu wenye bahati, wana ngekewa, wanafanikiwa, kumbe hicho ni kibali.

Watu wote wenye mafanikio yanayotokana na vipaji mbalimbali ni watu wenye vibali. Wafanyabiashara, wanafunzi na wasanii wenye vipaji vikubwa, wenye vibali wanafanikiwa na kuna watu huku mitaani wana vipaji vya ajabu sana lakini hawana vibali, hivyo hawatusui.

Jambo lingine tujiulize kama Nyerere, Mwinyi na Mkapa na Jakaya Kikwete walikuwa na vibali na walivitumia na kukamilika. Sala ya kuliombea Bunge huanza na neno "Mungu huweka serikali za mataifa". Kauli hii maana yake wakuu wote wa nchi huwekwa na Mungu, hivyo marais wote wa Tanzania kuanzia Mwalimu Nyerere hadi Samia Suluhu Hassan, wote wana vibali lakini vibali vya wengine ni virefu na wengine ni vifupi.

Rais wa awamu ya tano. John Magufuli, maarufu kama JPM, pia alikuwa na kibali lakini sina uhakika kama kilikuwa ni kibali kilikuwa kirefu cha miaka 10. Alikitumikia kibali chake kwa miaka mitano lakini alipoamua kujiongezea kwa kuufuata mtindo wa mserereko wa CCM, kibali hicho kikaondoshwa. Kibali chake kilikuwa kibali cha miaka 10, lakini hapa katikati akatofautiana kitu na mtoa vibali, hivyo mtoa vibali akaamua kukikatisha na kumpa Samia.

Swali lingine ni je, Rais Samia ni kibali? Jibu ni ndio, Rais Samia ni kibali, mapito yake toka alipoanza mpaka hapa alipofikia, kote kuna viashiria vyote kuwa huyu ni kibali. Swali la pili ni kibali cha nini na cha muda gani, hiyo ni Mungu tu ndie ajuaye.

Japo kibali kinatolewa na Mungu mwenyewe na kila anayepewa kibali, pia anapewa uwezo wa kutekeleza mahitaji ya kibali chake, lakini binadamu ni kiumbe dhaifu. Hakuna mkamilifu, hivyo kunaweza kutokea makosa ya hapa na pale na hakuna mtu anayeweza kufanya kila kitu yeye mwenyewe peke yake.

Kwa mantiki hiyo, ni lazima asaidiwe ndiyo maana japo Rais wetu ana kibali lakini ana wasaidizi wa kumsaidia kwenye kila eneo hata hivyo bado kunatokea makosa ya hapa na pale yakiwemo matukio yanayowatoa Watanzania machozi, jasho na damu, ambayo yanaweza kusababisha kufutwa kwa kibali chake.

Kwa vile kibali Rais Samia alichoingia nacho mwaka 2021 hadi 2025 ni cha JPM alichonyang'anywa akapewa ili kuimalizia ngwe ya Magufuli, sijui kama mtoa vibali anaukubali ule utaratibu wa mserereko wa CCM ndio maana licha ya JPM kuingia kumalizia kipindi chake cha pili kwa mserereko, mtoa vibali alikifuta.

Japo lengo la msesereko ni jambo zuri na lengo zuri la kuondoa kitu kinachoitwa 'duplicity' kwenye mchakato wa usaili wa ushindani wa wagombea urais ambao walisailiwa ili kumpata aliye bora, Rais Samia yeye hakusailiwa urais kwa ushindani. Kwa vile ameupata urais kwa kudra ya Mwenyezi Mungu, ni kibali kimemwepusha na ushindani, hivyo kwa mujibu wa utaratibu wa mserereko wa CCM, Rais Samia ndiye mgombea urais wa CCM wa mwaka 2025 kwa utaratibu wa CCM.

Kwenye mahojiano na Kikeke, aliposema 2025, twende na mwanamke, tumemuunga mkono ila tukamuulizia kuhusu kibali Watanzania tuunge mkono 2025 ni zamu ya Mwanamke. Kama ni yeye aliyepangiwa, basi na iwe hivyo.

**Mungu Ibariki Tanzania. Mungu Mbariki Rais Samia apate Kibali 2025 Paskali 0784 270403**

## KONA YA AFYA

# Maswali 10 yanayoulizwa zaidi kuhusu kisukari



Na Dk. Mabula Budodi

KISUKARI ni ugonjwa ambao huelezewa na namna mwili usivyoweza kuzalisha insulini mwilini au kutumia insulini iliyozalishwa mwilini vizuri.

Insulini ni homoni inayozalishwa kwenye kongosho na kazi yake ni kugeuza chakula kuwa nishati mwilini.

Hilo ndilo swali la kwanza ambalo huulizwa nini maana ya kisukari. Swali la pili ni lile kuhusu dalili ambazo humtokea mtu mwenye kisukari.

Dalili za mtu mwenye sukari ni pamoja na kuwa na njaa za mara kwa mara hata baada ya kula, kuwa na kiu ya maji hata baada ya kula, kukojoa mara kwa mara hata pasipo kunywa kiwango kingi cha maji, kupungua uzito kusikoelezeka kwa sababu ya haraka inayoeleweka na hata kuwa na uoni hafifu ambao huongezeka siku kwa siku.

Lakini si kweli ya kwamba watu wote watatokewa na dalili tajwa hapo juu bali muda mwingine huweza kutokuwa na dalili zozote na kutokea dalili za kuchelewa kama kuwashwa sehemu za siri, kuuma mara kwa mara kunakosababishwa na bakteria, kutokupona majeraha na vidonda kwa haraka, kupata ganzi miguuni, mikononi na hata kuhisi pini kuchoma choma miguuni au mikononi.

Swali la tatu, ni namna gani unaweza kugundua kama una tatizo la kisukari? Namna pekee unaweza kugundua kama una tatizo la sukari ni kupima kiwango chako cha sukari mwilini, yaani kuwa na kiwango kikubwa cha sukari ya mfungo zaidi ya saa nane itayokuwa zaidi ya 7mmol/l. Kiwango cha sukari kwenye damu kinachozidi 11.1 mmol/l baada ya kupewa kiwango cha 75g na kiwango cha zaidi ya asilimia saba cha sukari ya miezi mitatu.

Je ni watu gani wako kwenye hatari zaidi ya kupata tatizo la sukari?

Jibu ni kwamba watu walio na historia ya kuwa na tatizo la kisukari kwenye familia, yaani watu walio na ndugu wa karibu wa kuzaliwa nao wenye sukari wako katika hatari mara mbili hadi tatu zaidi kupata kisukari. Watu walio na wazazi wawili wenye tatizo la kisukari pia wana hatari mara tano zaidi ya kupata kisukari.

Ukiwa na unene uliopitiliza pia unaweza kuwa katika hatari ya kupata kisukari kwa sababu husababisha mwili kushindwa kutumia insulini yake vizuri kumeng'enya chakula, hivyo kusababisha kuchakata pia sukari mwilini na kusababisha ongezeko la sukari mwilini maradufu.

Kuwa na tatizo la sukari ya mimba, huchangia kupata sukari baadaye. Mfumo wa maisha, yaani kuvuta sigara, kutokufanya mazoezi, kupenda vyakula vya sukari nyingi, kunywa pombe kwa wingi pia ni chanzo cha mtu kupata sukari.

Je, ni mambo gani hupunguza na kuongeza kiwango cha sukari mwilini kwa watu wenye kisukari? Mambo yanayoweza kusababisha kushuka kwa kiwango cha sukari mwilini zaidi kupita kiasi ni kuchoma kiwango kingi cha insulini, kuruka chakula, yaani cha mchana au cha usiku, kunywa pombe, kufanya shughuli za kutumia nguvu zaidi na pia kunywa dawa za sukari nyingine huku ukiwa unachoma insulini zinazoweza kushusha sukari zaidi.

Vitu vinavyoweza kuongeza kiwango cha sukari zaidi mwilini ni pamoja na kuumwa, kuwa na msongo wa mawazo, kuchukua au kuchoma kiwango kidogo cha insulini tofauti na kile kinachotakiwa, kula kiwango kikubwa zaidi ya kinachotakiwa hasa wanga kwa wingi.

Mtu akiwa na tatizo la kisukari anatakiwa kutotumia kabisa vyakula vya wanga? Jambo hili limewachanganya watu wengi. Jibu ni kwamba si kweli bali wanapaswa kupunguza kiwango cha wanga kwenye chakula na kula kiwango kinachohitajika tu mwilini. Ni kweli ubongo na mwili pia huhitaji chakula aina ya wanga ili kufanya kazi zake za kila siku vizuri bila hivyo waweza kukosa nguvu za kufanya kazi zako za kila siku.

Ulaji unaotakiwa kufuatwa ili kuwa na kiwango cha sukari kinachotakiwa mwilini kudhibiti kiwango cha sukari. Njia hii huhusisha kuhesabu kiwango cha wanga anachokula mtu kwa kuangalia lebo za vyakula na hata pia kupima kiwango cha wanga anachokula kabla ya kukila. Njia hii huhusisha kujifunza na hesabu mbalimbali ambazo hubidi kujifunza aina vya vyakula na kiwango chake cha wanga.

Hata hivyo, kiwango cha wanga ambacho mwili utahitaji kufanya kazi vizuri na kutokupandisha kiwango cha sukari mwilini ni jambo la muhimu .Hii yote itafanyika baina ya mtu na mtaalamu wa lishe wako na huchukua miezi kadhaa mpaka kuwa na utaalamu tosha kwenye swala hili.

Kwa hiyo aina rahisi ambayo watu wengi wanaweza kufuata ni kudhibiti kiwango cha ulaji wanga kwa kutumia ulaji wa njia ya sahani ya chakula ya kila siku. Mtu inabidi atumie sahani ya inchi nane angalau maana kuna sahani za inchi 12 na kuendelea ambazo zitakuwa kubwa sana.

Inapaswa kwenye sahani hiyo nusu kuweka chakula aina ya mboga na matunda ukiunganisha vyakula vizima visivyopondwa pondwa au kusagwa. Robo ya sahani inapaswa kuwekwa chakula aina ya protini, yaani mayai, nyama samaki, kuku, mtindi, karanga na maharage. Robo iliyobakia kwenye sahani ihusishe chakula aina ya wanga yaani wali, ugali, ulezi, mtama, mahindi kwa maana ya nafaka.

Mtu pia anashauriwa kupendelea nafaka isiyosagwa au kuponda ponda ikiwa nzima nzima ili kuzuia kupanda kiwango cha sukari ghafla mwilini.

Mtu anaweza kudhibiti kiwango cha sukari mwilini kwa kula vizuri, kufanya mazoezi na kuthibiti uzito mwilini. Hii inahusisha kula katika muda unaotakiwa na kutokuruka mlo.

Pia kula matunda mazima na maji badala ya juisi na soda, kufanya mazoezi mara kwa mara angalau dakika 30 kwa siku ndani ya siku tano za wiki. Pia inashauriwa kupunguza unywaji pombe na kuacha kama inawezekana.

Muda mtu anaotakiwa kuangalia kiwango cha sukari mwilini ni baada ya kuamka kutoka kitandani, kabla ya kula, saa mbili baada ya kula na kabla ya kwenda kulala.

Kuhusu vyakula na vinywaji visivyo na sukari, mtu anaweza kutumia kiwango kidogo tu maana bado hata vyakula na vinywaji ambavyo havina sukari huwa na kiasi fulani cha wanga, hivyo vinapaswa kutumika katika kiwango maalumu.

**•Dk. Budodi ni daktari wa binadamu anapatikana Dar es Salaam. Unaweza kuwasiliana naye kwa namba 0710 980096 au barua pepe mabulabododi@gmail.com**

# Chai ya Tanzania yapata sifa Japan

**Na Halfani Chusi,** MUFINDI

UJUMBE wa watu watano kutoka Japani ulioongozana na kampuni mbili za chai umeimwagia sifa chai ya Tanzania na kuahidi kuja kufanya uwekezaji.

Kampuni hizo ni Kawasaki na Nara Cooperation ambazo zimekuja kutoka Japani, kuangalia fursa katika zao la chai na kubadilishana uzoefu.

Sifa hizo zimetolewa juzi na Mkurugenzi Kitengo cha Maendeleo Kawasaki, Hirofumi Suganuma, baada ya kutembelea Kituo cha Utafiti wa Chai Tanzania (TRIT) na mashamba ya mkonge AMCOS, ikiwa ni mwendelezo wa ziara yao ya kutembelea mashamba ya chai na kuangalia fursa zilizopo.

"Chai ya Tanzania ni nzuri, na tumeona ile yenye majani membamba ambayo ndio inahitajika zaidi Japani kwa ajili ya kutengeneza chai ya kijani.

"Lakini pia mitambo tuliyonayo inaweza kuichakata majani ya chai membamba hata yenye majani mapana nayo ni nzuri," alisifu.

Aliwasihi wakulima waendelee kufanya uwekezaji katika chai ya majani membamba na kwamba ina soko kubwa Japani.

Wakati wanakagua chai katika eneo hilo, walikuwa wanaipima kwa kutumia tepu kwa lengo la kwenda kulinganisha na mashine zao kuona kama ukubwa au udogo wake hautaathiri mashine zao wakati wa kuchakata.

Ofisa Kilimo Idara ya Maendeleo ya Mazao Wizara ya Kilimo, Bahati Majaliwa, alisema mpango wa serikali ni kujenga viwanda vidogo vidogo vitakavyo wasaidia wakulima kusindika chai ili waweze kupata faida zaidi kutokana na mauzo.

"Wajapani wameipenda sana chai yenye majani membamba na inazalishwa kwa wingi, katika maeneo mengi ya uzalishaji hapa nchini, ikiwamo yale ya mkonge lakini nchini kwetu ni zaidi ya asilimia 80 ya chai hiyo inazalishwa nchini.

"Wakulima waendelee kutunza mashamba yao vizuri ili kupata tija kutokana na majani watakayozalisha" alisema Majaliwa

Alisema mkakati wa wizara kwa sasa ni kuhakikisha wakulima wanasindika chai yao na kwamba kilichopo kwa sasa ni kuwekeza katika viwanda vya wakulima wadogo.

"Bado Wizara ina nia ya kuhakikisha uwekezaji viwanda unafanyika ili wakulima waweze kusindika chai.

"Wakulima wa chai watambue serikali inaendelea na jitihada kuhakikisha zao la chai linaendelea hapa nchini kwa kuweka viwanda vya wakulima wadogo," alisema Majaliwa.

Alisisitiza kuwa ujenzi wa viwanda kwa wakulima wadogo utasaidia kuwainua kiuchumi na kuzalisha chai yenye tija na itakayoleta ushindani katika soko la kitaifa na kimataifa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utafiti wa Chai Tanzania (TRIT), Dk. Daniel Mgori alisema ujio wa ugeni huo katika kituo chao umewapa somo kubwa na kujua aina ya chai inayohitajika Japani.

Aliwahakikishia Wajapani kwamba taasisi itafanya jitihada za kuzalisha miche ya aina ya chai wanayoitaka ili wakulima waweze kulikamata soko lao.

Alisema kampuni zilizowatembelea zimeongozana na wataalamu wa kutengeza mashine za kuchakata chai na wamewapa ushauri wa namna ya kulima zao hilo.

Mwenyekiti wa mashamba ya Mkonge Amcos, Balodaniel Mgonzo aliomba wajengewe kiwanda ili waachane na adha ya kuuza majani mabichi jambo linalowasababishia hasara.

Alisema tayari wametenga kiwanja chenye ukubwa wa hekari 12 ili atakapopatikana mwekezaji awajengee kiwanda waweze kukuza majani makavu.

Alisema kwa sasa wanakabiliana na changamoto ya malipo kidogo, ukilinganisha na gharama za uendeshaji wa mashamba

"Tunawakaribisha Wajapani waliokuja kututembelea leo wajenge viwanda vyovyote wanavyotaka na kama eneo tulilotenga halitatosha bado kuna eneo jirani wakulima wapo tayari kujitolea"



Mchuuzi wa kinu cha kutwangia na kibao cha kukunia nazi akiwa amepanga bidhaa zake katikati ya eneo la hifadhi ya barabara ya Morogoro Chalinze mkoani Pwani huku akipatana na wateja wake hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# CCM yawatia moyo vijana wenye sifa kupata vyeo

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Singida, kimewatia moyo vijana mkoani humo kujiimarisha na kuwa waaminifu, kwa kuwa ndio chama ambacho kinaweza kumtunuku mtu yeyote cheo kulingana na sifa alizokuwa nazo.

Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM, Mkoa wa Singida, Dk. Denis Nyiraha, akizungumza juzi wakati akifungua mkutano wa Baraza la Vijana wa CCM, Wilaya ya Iramba, alitaka vijana kuendelea kujitangaza kwamba, wao ni viongozi wa kesho na asitokee mtu atakayewakatisha tamaa.

"Vijana tunaweza tukawa yeyote katika nchi hii, kinachohitajika ni maandalizi yetu ya leo ndio yatatufanya tuwe nani katika nchi hii. Endeleeni kujiamini, kufanya kazi kwa bidii na kuishi ndani ya CCM," alisena Nyiraha aliyemwakilisha mgeni rasmi, Mbunge wa Iramba Magharibi, Dk. Mwigulu Nchemba.

Alisema jambo la msingi la kuzingatia ni kuendelea kuwa waaminifu ndani ya chama.

Alisema haiwezekani unasema unataka uende mbinguni wakati huamini kama Mungu yupo na haujui mlango wa msikiti wala wa kanisa.

"Muulizeni Dk. Mwingulu miaka 25 iliyopita alikuwa nani. Unaweza kukata tamaa sana kama utamuona Dk. Mwigulu miaka 25 alikuwa anazoa uchafu kwenye zizi la ng'ombe, lakini leo ni Waziri wa Fedha kwenye nchi ya Tanzania," alisema.

Katibu wa Umoja wa Vijana (UVCCM), Wilaya ya Iramba, Amani Clement, alisema katika kuhakikisha umoja huo unajikwamua kiuchumi na kuondoka na utegemezi, kuna mpango wa kuanzisha mradi wa kuosha magari eneo la Misigiri ambao utagharimu Sh. milioni 6.5.

Clement alisema changamoto zinazoukabili umoja huo ni kutokuwa na usafiri kwa ajili ya viongozi ngazi ya wilaya, umaliziaji wa ujenzi wa nyumba ya mwalimu kukwama ambapo zinahitajika zaidi ya Sh. milioni 19 na ofisi ya UVCCM kuwa na samani ambazo zimechakaa zinahitajika Sh. milioni 1.5 kununua mpya.

"Tunamshukuru mbunge wetu Dk. Mwigulu katika ujenzi wa nyumba ya Katibu wa UVCCM, ametusaidia sana na pia tunamwomba aendelee kutusaidia mambo mengine ambayo tunayahitaji," alisema.

# Serikali imeingia makubaliano na TLS kushughulikia rufani za wafungwa

**Na Idda Mushi,** KILOMBERO

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Damas Ndumbaro, amesema kupitia Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia Legal Aid wameingia mkataba na Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS), ili kuwafikia wafungwa magerezani kushughulikia changamoto zikiwamo za rufani.

Waziri Ndumbaro aliyasema hayo wilayani Kilombero, mkoani Morogoro, wakati akizungumza na wafungwa walioko katika Gereza la Kiberege, wilayani humo.

Alisema jopo la mawakili kutoka TLS litawafikia wafungwa katika magereza mbalimbali nchini.

"Maelekezo hayo ni maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan kuhakikisha wafungwa na mahabusu wanapata haki zao na kwamba, mawakili hao pamoja na mambo mengine, watawasaidia kuandika rufani kwa wenye malalamiko ili kuzipeleka mahakamani," alisema.

Kuhusu maombi ya baadhi ya wafungwa kutaka wahamishwe magereza kupelekwa jirani na nyumbani kwao, Waziri Ndumbaro alisema, kufungwa ni adhabu, hivyo ni vyema wakaachana na mawazo ya kuchagua gereza, kwani Tanzania ni moja na kila mtu ana haki ya kuishi popote.

"Kuhusu makosa ya msamaha, mtambue kuwa msamaha unaendana na matendo mazuri utakayotenda wakati wa kifungo gerezani.

"Yapo makosa makubwa ambayo hayana dhamana kama uhaini, mauaji, kujamiiana, ubakaji na uhujumu uchumi, niwaombe Watanzania kujiepusha na makosa haya ili mbaki salama," alisema.

Waziri Ndumbaro aliwaagiza watendaji wa wizara hiyo kufunga vifaa vitakavyotumika kusikiliza kesi za wafungwa kwa njia ya mtandao, ili kukabiliana na changamoto ya mahabusu kutopelekwa magerezani.

"Tayari mahakama zimeingia katika mfumo wa kimtandao, hii itasaidia wafungwa na mawakili kusikiliza kesi mbalimbali wakiwa katika magereza yao, badala ya kusafiri kwenda mahakamani," alisema,

Awali, baadhi ya wafungwa walilalamikia changamoto ya kukosa msaada wa kisheria katika gereza hilo, jambo linalowafanya kushindwa kutekeleza rufani zao na kupoteza haki zao za msingi.

Pia walimwomba Rais Samia kuongeza idadi ya watu wanaopewa msamaha magerezani, kwani kwa sasa ni wachache na wanapata fursa hiyo.

Kadhalika walilalamikia kitendo cha ucheleweshwaji wa kupelekwa mahakamani na hivyo kesi kuchukua muda mrefu, sambamba na kuwalalamikia baadhi ya askari kuwapiga pindi wanapowakamata na kuwalazimisha wakubali makosa

# MAISHA

DESEMBA 15, 2024

Nipashe


Baba, Mama na Mwana

Jumapili




HARUSI

Ukurasa 12




## Kunjua ngozi ya uso

Ukurasa 14

# WATOTO

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA




| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 4 | 3 |
| 3 | 4 | 1 | 2 |
| 2 | 1 | 3 | 4 |
| 4 | 3 | 2 | 1 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | M | A | L | I | | T |
| | | | | N | | U |
| T | | S | U | D | A | N |
| O | | P | | I | | I |
| G | H | A | N | A | | S |
| O | | I | | | | I |
| | A | N | G | O | L | A |


## FUMBO TOTO

Haya, hebu tuone umahiri wako wa somo la Kiingereza shuleni; jaza majina haya ya wanyama kwa Kiingereza katika fumbo letu.


NG'OMBE, CHUI, PAKA, FARASI, MBUZI, NYANI, POPO



## TOA TOFAUTI 5



## PAKA RANGI




## AMSHA AKILI

LOOOOH! MAKINDA MATATU YA MAMA NDEGE YAMEKWENDA WAPI JAMANI? HEBU TUMSAIDIE KUYATAFUTA!



## CHEKA



Alichokifanya daktari

TOFAUTI ya wazazi wa hapa nchini mtoto wa Tanzania na sehemu zingine wakati anapolala inakuwa kama hivi.

Marekani mtoto anapokwenda kulala huagwa na wazazi wake "usiku mwema mwanangu"

Uingereza wazazi wanamuaga mtoto wao "Pata njozi njema mwanetu"

Hispania anapokwenda kulala wazazi humuambia "usiku mwema mpendwa wetu"

Tanzania mtoto anapotaka kulala wazazi utawasikia "Kesho uamke mapema, hatutaki kusikia umechelewa na hela ya mihogo utaikuta mezani"

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Hiki ndicho chanzo cha matatizo ya ndoa nyingi

KARIBU tena msomaji wangu tuendeleze mada kuhusu mitikisiko katika ndoa nyingi hata kusababisha zingine kubomoka na kila mwanandoa kuanzisha maisha mengine.

Wiki iliyopita tulijadili kwa nini shetani anashambulia sana ndoa? Nilitaja maeneo mawili, moja likiwa ni ujinga kwa baadhi ya wanandoa kutokuwa na maarifa namna ya kuishi katika ndoa.

Nikataja kupuuzia kanuni na misingi ya ndoa. Ukitaka uwe na ndoa yenye mafanikio na upenyo ni lazima utendee kazi kanuni na maelekezo yote yanayohusu ndoa.

Kwa bahati mbaya sana, watu wengi walioko kwenye ndoa hupuuza na kutupilia mbali kanuni na maelekezo waliyopewa siku wanafunga ndoa. Unapopuuzia kuombea ndoa yako, unapoanza kuona mabadiliko kwa mumeo au mkeo unapuuzia, hiyo itakugharimu baadaye.

Unapoota ndoto mbaya kuhusu mumeo au mkeo na kupuuzia, unaweza kujikuta unaingia kwenye matatizo makubwa ya ndoa baadaye.

Leo msomaji wangu tuende zaidi kuangalia chanzo cha matatizo ya ndoa. Nitajitahidi kuchambua vyanzo mbalimbali kadiri itakavyowezekana ili kusaidia wanandoa wengi ambao wana maswali mengi kuhusu mitikisiko katika ndoa zao wasijue cha kufanya.

Ni vema ikaeleweka kwamba kila tatizo la ndoa lina chanzo. Moja ni zile ndoa zinazofanyika pasipo Mungu kuhusika. (wakati ulikuwa adui wa Mungu). Watu wengi ambao huanza maisha ya ndoa pasipo kumshirikisha Mungu hukumbana na matatizo makubwa ya ndoa.

Siku zote msingi mbaya wa nyumba husababisha jengo kuwa dhaifu. Uhusiano wowote uliofanya wakati ukiwa adui wa Mungu huwa unafeli.

Mwanaume yoyote aliyeokoka na kuchukua maamuzi ya kumuoa binti ambaye hajaokoka, hujisababishia matatizo yeye mwenyewe huko baadaye. Ipo hivyo pia kwa binti kuolewa na mtu asiyeamini upo uwezekano wa matatizo baadaye.

Ndiyo maana Mungu akasema katika moja ya maandiko yake kwamba, "Msifungiwe nira pamoja na wasioamini, kwa jinsi isivyo sawasawa; kwa maana pana urafiki gani kati ya haki na uasi?"

Chanzo kingine ni pale ndoa inapofungwa kwa sababu tu ya kupata mimba kwa bahati mbaya/kumpa binti mimba. Watu wengi leo wameoana siyo kwa sababu walipenda, bali kwa sababu walilazimishwa kutokana na kupeana mimba kwa bahati mbaya.

Ndoa za aina hiyo hazifanyiki kwa sababu ya upendo bali kwa sababu ya matokeo ya kile walichokifanya. Aina hii ya ndoa inaitwa "zimamoto". Kama umewahi kuona watu wa zimamoto wanavyofanya kazi kwa haraka sana na hawana muda wa majadiliano.

Binti anapopata mimba tu, kila mtu huanza kutaharuki. Wazazi wa pande zote mbili hukaa kwa haraka na kukubaliana ndoa ifungwe kwa haraka sana ili wasipate aibu.

Aina hii ya ndoa hutokana na tamaa ya mwili na siyo upendo wa dhati. Kama ungekuwa ni wa kweli binti asingejikuta ameingia katika matatizo ya namna hiyo.

Chanzo kingine ni kujihusisha kimapenzi kabla ya ndoa. Imebainika kwamba mapenzi kabla ya ndoa husababisha matatizo makubwa sana ya ndoa leo na kufanya mtu ajijengee majeneza ya kuzimu. Kama ukijenga jeneza kwa ajili ya ndoa yako, lazima utazikwa huko!

Vijana wengi leo wameshindwa kutunza ujana wao. Mabinti wengi nao wanaaibisha wazazi wao. Wengi wanaingia vyuoni, lakini wanapohitimu wanakuwa ni makahaba waliofuzu!

> **"Nikataja kupuuzia kanuni na misingi ya ndoa. Ukitaka uwe na ndoa yenye mafanikio na upenyo ni lazima utendee kazi kanuni na maelekezo yote yanayohusu ndoa.**

Chanzo kingine kinatokana na ndoa zilizofungwa baada ya mtu kwenda kwa mganga wa kienyeji. Ni kawaida katika tamaduni za baadhi ya wazazi wa Ki-Afrika kutembelea waganga wa kienyeji ili wawabashirie hatma za watoto wao.

Na mara zote, watu wengine wanaoamini huenda kwa wazazi wao na kuwaambia kwamba Bwana amewaongoza kuoa watu wa aina fulani. Ndipo wazazi huchukua majina ya wachumba wao na kuyakimbiza kwa waganga ili wajue kama ni mke/mume sahihi wa watoto wao.

Kama wewe ni mchunguzi msomaji wangu, wazazi wengi wa ki-Afrika, wana tabia ya kuchukua majina ya watu wanaowazunguka watoto wao. Kama ndoa yako ilifanyika katika misingi hiyo, haitafika mbali. Shetani ni mjanja sana. Anatumia historia ya maisha yako kupambana na maisha ya ndoa.

Leo tuishie hapa tuendelee wiki ijayo, nikutajie vyanzo vingine zaidi vinavyotesa ndoa nyingi katika jamii yetu. Bila shaka umejifunza kitu hapo.

**Je, una maoni au kisa cha kimaisha? Ujumbe mfupi 0715268581.**

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Ukweli mchungu usiosemwa kuvunjika ndoa

WANAWAKE mkoani Kilimanjaro wanatajwa kuwa vinara wa kuvunja ndoa nyingi kwa mikono yao.

Leo nitajikita zaidi kuzungumzia marejeo ya habari hiyo niliyoichapisha katika Nipashe Digital, ikiwa na kichwa kisemacho, "Wanawake waongoza kwa kivunja ndoa Kilimanjaro'.

Kuna uhusiano mkubwa sana kati ya mwanamke kuimarika au kupata uhuru wa kiuchumi na kupoteza uwezo wa kuwa mke. Ni ngumu sana mwanamke kujitosheleza kiuchumi na kutii mamlaka inayoitwa mume. Ni vizuri wanaume wa karne hii wakaelewa hili.

Mmoja wa watu walioguswa na kichwa cha habari hiyo, aliyejitambulisha kama Deo Sukambi, ameandika katika ukurasa wa maoni wa IPP Media kwamba mwanamke akipata uhuru wa kiuchumi anatamani kuwa huru.

Ameandika kwamba hilo ni jambo la asili tu hata wanaume iko hivyo. Tatizo ni kwamba hawezi kuwa huru na akawa mke kwa wakati mmoja. Ni rahisi kuwa mume na kuwa huru ila kinyume chake sio rahisi.

Je, wanawake hubadilika wanapopata pesa? Si suala la kubadilika bali pesa ina nguvu ya kumfanya mtu atake kuitumia anavyotaka. Sasa anaitumiaje wakati hana uhuru kwa sababu kaolewa?

Uamuzi wa haraka atakaofanya ni kumuasi mume ama kwa kumshurutisha kumpa uhuru wake au mke kujipangia mfumo, kiwango au utaratibu wa maisha yake ndani ya nyumba. Mume akigoma, ama ndani hakutakalika au ndoa itavunjika.

Je, wanawake hawapaswi kuwa na uhuru wa kiuchumi? Si kweli, Ni vyema mwanamke akayamudu maisha yake kiuchumi hata kabla ya kuolewa ili kuondoa uwezekano wa kuolewa. Hiyo ni kwa sababu akishindwa kujimudu kiuchumi hilo nalo ni hatari.

Kipimo kimojawapo kikubwa kuwa mwanamke anafaa kuwa mke ni kuwa na uhuru wa kiuchumi na akatamani kuwa mke (si akatamani kuolewa, anaweza akatamani kuolewa ila hataki kuwa mke).

Ukikutana na mwanamke ambaye anajimudu kiuchumi na amekuwa mke mheshimu sana maana huyu amefikia kiwango cha juu cha utu wake wa asili.

Yule ambaye ni mtii lakini hana uhuru wa kiuchumi usiwe na uhakika sana akipata uhuru huo ataendelea kuwa mtii.

Deo ameandika angalizo akisema si wanawake wote hushindwa kuwa mke kwa kupata uhuru wa kiuchumi lakini ni wachache sana waweza kufikia ukomavu huo wa kutengeneza uwiano sahihi kuhusu nafasi ya mke na shauku ya kuwa huru, kwa sababu ya kuimarika kipato chake.

Nilikutana na mchango huu, baada ya kuandika kuhusu jukwaa la wanaharakati wa kupambana na ukatili wa kijinsia mkoani Kilimanjaro, kufichua siri kuwa migogoro mingi ya ndoa inayoibuka kila uchao mkoani humo, inasababishwa na baadhi ya wanawake ambao vipato vyao vimeimarika, kutokuwa na heshima katika ndoa.

Huku wanawake hao wakiwa hawaoni sababu ya kushiriki tendo la ndoa na wenza wao.

Nilimnukuu Msemaji wa mashirika 12 ya kiraia yaliyotoa tamko la kulaani ukatili huo, Wakili mkongwe nchini na mwanaharakati wa haki za binadamu, Elizabeth Minde.

Wakili Minde anasema kundi rika la miaka 30 hadi 45 ya wanawake ndilo ambalo limeonekana kulalamikiwa sana maeneo mbalimbali.

"Wengine wakisema: 'Hawa wapora wadogo (mke mdogo) wanawaonea sana waume zao' mfano halisi ni nukuu kutoka katika mjadala wa kijamii uliofanyika kata ya Mwika Kaskazini.

"Sisi wanaharakati tunasema kuwa kuimarika kwa kipato cha mwanamke kisiwe chanzo cha migogoro ya ndoa. Muhimu ni kuimarisha mawasiliano, mahusiano na maamuzi shirikishi katika bajeti za familia, matumizi ya muda kwa uwazi na uwajibikaji wenye ustawi chanya na ulio endelevu ndani ya familia."

Aidha, wanaharakati hao wameeleza kiini cha migogoro hiyo pia kinachagizwa zaidi na kuimarika kwa fursa za kiuchumi kwa wanawake wa Mkoa wa Kilimanjaro.

Kwa mujibu wa Wakili Minde, wanawake wengi wa mkoa huo kwa sasa ni wafanyabiashara wakubwa, wa kati na wengi wao ndio wenye mitaji katika masoko makubwa kama Soko la Kumbukumbu ya King George (Memorial) na kwa Sadala.

Anasema wanawake katika wilaya za Rombo na Halmashauri ya Moshi ni mifano ya wanunuzi na wauzaji wakubwa wa mazao ya biashara kama ndizi, parachichi na bidhaa nyingine mfano maduka ya nguo, ikilinganishwa na miaka ya 1995.

Nimeandika haya magumu katika ndoa, kwa sababu kumekuwa na mikinzano kuhusu usuli wa Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 na mikataba ya kimataifa kuweka shinikizo.

Haya ya wanawake yanajitokeza wakati ambapo, dunia ikielekea katika miaka 30 ya Beijing, inayotanguliwa na kauli mbiu chagua kutokomeza ukatili wa kijinsia.

Ingawa, mashirika ya haki za binadamu, asasi za kiraia na wadau mbalimbali, wako katika mapambana ya kupinga vitendo hivyo; kuna mapokeo chanya katika maeneo mengi nchini Tanzania.

**•Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com**

# HARUSI



Ni harusi ya kipekee kiasi ambacho walioudhuria walionekana kuwafurahia maharusi ambao walibatizwa jina la KingTan. Sherehe hiyo ilifanyika jijini Dar es salaam hivi karibuni na kutumbuizwa na kundi la muziki la Akili The Brain. PICHA: MC GaraB

MITINDO

Na Moshi Lusonzo



# USICHANGANYIKIWE Vaa kilicho bora

KUCHAGUA nguo nzuri dukani ni jambo lenye changamoto nyingi, wakati mwingine unaweza kuchanganyikiwa na usijue nguo gani unataka.

Hata hivyo, usiwe na hofu kwani leo utapata vidokezo ambavyo vitakusaidia kuangalia nguo bora unapokwenda dukani.

**UBORA WA KITAMBAA**

Suala la kitambaa ni jambo la kuzingatiwa wakati wa kuchagua nguo. Unatakiwa kuhakikisha unapata nguo yenye kitambaa chenye ubora mzuri na kinachoweza kudumu kwa muda mrefu.

**MITINDO MUHIMU**

Chagua nguo yenye mtindo unaoupenda na unaolingana na umbo lako la mwili. Kama shati angalia mtindo gani unataka na linalokukaa vyema.

**RANGI YA NGUO**

Ngozi ya mwili inaendana na rangi ya nguo unayochagua, hakikisha rangi ya nguo haitaondoa mvuto na haiba yako.

**UKUBWA WA NGUO**

Hakikisha unapata nguo yenye ukubwa unaokufaa. Usichague nguo kubwa sana au ndogo sana. Hakikisha unajaribu nguo ili kuhakikisha inakufaa vizuri.

**BEI NAFUU**

Gharama inayolingana na bajeti yako ni kitu cha kuzingatia unapokwenda kununua nguo. Angalia unafuu unaweza kuharibu ubora wa nguo unayohitaji kununua.

URUMBO

Na Mary Geofrey

# Kunjua ngozi ya uso



UNAWEZA kutumia matunda na namna nyingine ya mimea kuondoa mikunjo usoni kwako.

Wiki iliyopita tulielezana baadhi ya matunda na mimea na leo hii tunaendelea tulipoishia lengo ni kuhakikisha unakuwa mrembo wakati wote.

**Aloe Vera**

Jeli ya Alovera inatakiwa katika kuondoa mikunjo kwenye uso wako. Chukua jani lake na kisha likate ili kupata utomvu wake.

Chukua utomvu au jeli hiyo kama wengine wanavyoita na kisha pakaa sehemu iliyoathirika, itapunguza ama kuondoa kabisa tatizo hilo.


**Parachichi**

'Maski' ya Parachichi husaidia kuifanya ngozi iwe na mng'ao. Siyo hivyo tu, bali huchangia kwa kiasi kikubwa pia kuifanya ngozi iwe laini na nyororo.

**Jinsi ya kutumia**

Chukua parachichi lililoiva vizuri, kisha saga hadi lilainike.

Baada ya hapo pakaa sehemu iliyoathirika na acha kwa muda wa dakika 10, kisha osha sehemu hiyo uikaushe.



**Papai**

'Maski' ya Papai pia husaidia kuondoa tatizo hili.


**Unachotakiwa kufanya**

Chukua kipande cha papai kilichoiva na kuchanganya na kijiko kimoja cha unga wa ngano.

Pakaa sehemu iliyoathirika na kaa nayo kwa muda usiopungua dakika 10. Mbali na kupaka pia unaweza ukatumia kula kwa sababu lina vitamin E kwa wingi, ambavyo ni muhimu katika ukuaji wa ngozi.

**Danzi**

Juisi ya tunda hili husaidia katika uzalishaji wa sehemu ya juu ya ngozi 'collagen'. Danzi lina kiwango kikubwa cha vitamini C. Na kwa kawaida aina hii ya vitamin husaidia kuchochea ukuaji wa 'collagen', hivyo kuifanya ngozi yako kunawiri.



MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Pilau la kuku wa kukaanga





SIKUKUU ili inoge ukiwa nyumbani lazima kuwa na pilau ambalo ni chakula kitamu na kila mtu anapendelea kula na soda yake pembeni.

Sikukuu hii ya Krismasi acha nikuelekeze namna ya kupika pilau la kipekee la kuku rosti ya ukafurahia vizuri mlo wako.

**Mahitaji**

Kuku mmoja kwa pilau kilo moja na nusu, soya sosi, chumvi, mafuta, mchele, viazi kiasi, njegere kiasi, vitunguu maji na vitunguu saumu.

**Namna ya kupika**

Anza kuandaa kwa kuosha kuku wako na waweke viungo vyako tayari kwa kuchemsha kidogo hadi waive na uweke pembeni baada ya kupokea zikate vipande kidogo.

Baada ya hapo anza kuandaa vya kupikia Pilau na anza kuchemsha kwanza maji, baada ya hapo tenga sufuria jikoni, weka mafuta yakipata moto anza kutumbukiza kuku wako uliowachemsha awali wakaange hadi wakianza kubadilika rangi iweke vitunguu maji viive pamoja hadi kuwa kahawia.

Baada ya hapo zitoe kuku kwenye mafuta na weka chombo cha pembeni na kisha anza kupika pilau kwa kukaanga vitunguu maji na vitunguu saumu kutimia mafuta hat ohayo, weka na viungo vingine, njengere, viazi na viungo vya pilau kisha vikiwa kahawia weka maji ya kupikia pilau yakicheka uweke mchele wako na funikia uchemke.

Ukiiva geuza wali wako vizuri na weka nyama za kuku na na changanya na pilau, funikia kwa muda na epuka litakuwa tayari kwa kuliwa na kachumbari pembeni.

# Krismasi isipite bila pambo

Na Restuta James

ZIMESALI siku tisa pekee kufikia sikukuu ya Krismasi. Ukitembelea maduka makubwa utaona walianza kupamba tangu Novemba Mosi, ikiwa ni matayarisho ya sikukuu za mwisho wa mwaka.

Kama bado hujaipamba nyumba yako, usiwe na wasiwasi, unaweza kutumia bajeti ndogo kubadilisha mandhari ya nyumba yako katika siku chache zilizobakia.

Mtaalamu wa bustani ambaye pia ni mbunifu wa mapambo ya nyumba, Anastela Thomas, anasema sikukuu ya Krismasi inaambatana na mambo mengi, mojawapo likiwa ni pambo la mti wa sikukuu hiyo.

Anasema kwa wenye bajeti ndogo, sio lazima wanunue mti katika wakati huu ambao bei inakuwa juu, bali wanaweza kununua mapambo mengine ambayo yatapendezesha nyumba.

Anasema kwa wenye uwezo, wanaweza kuzingatia miti au pambo la rangi wazipendazo na kuzichanganya au wakatumia aina moja ya rangi na nyumba ikaonekana nadhifu.

Mathalani, anasema mtu anaweza kutumia mapambo ya rangi ya bluu, kijani, nyekundu, nyeupe, dhahabu au fedha, kila moja ikijitegemea au akachanganya walau rangi mbili au zaidi.

"Kila rangi hapo inaweza kusimama peke yake, lakini zote pia zinaweza kuchanganywa hata tatu. Inategemea mtu anapenda rangi gani zaidi. Mfano nyeupe tupu, kijani, bluu au nyekundu. Ukichanganya ni sawa au ukitenganisha pia hakuna shida," anafafanua Anastela.

Anasema mwenye nyumba anaweza kupamba kuanzia mlangoni, kwenye korido, meza ya chakula, vyumbani na hata kwenye maliwato pamoja na eneo la bustani.

"Unaweza kutumia mishumaa, glasi na maua ya asili kupamba. Ukishindwa kabisa unaweza kupamba walau meza ya chakula ili familia ifurahie pamoja wakati wa sikukuu," anasema.

Hata hivyo, anashauri kwamba maandalizi ya kupamba Krismasi, yanatakiwa ya yaanze mapema kwani ni tukio linaloambatana na likizo ndefu kutokana na sikukuu za mwisho wa mwaka ambazo zinakutanisha familia.



MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Ifanye nyumba iwe nyumbani, kila mtu afurahie sikukuu za mwisho wa mwaka

MIONGONI mwa maeneo ambayo huwa ni faraja na ya kupumzisha akili baada ya shughuli nyingi ni nyumbani.

Nyumbani ndipo palipo na mkusanyiko wa maisha, kumbukumbu na upendo kwa asilimia kubwa ya watu.

Binadamu kila mmoja hujishughulisha na mambo mbalimbali lengo likiwa kujitafutia riziki na kuhakikisha mkono unakwenda kinywani na mambo mengine ya kifamilia yanakwenda sawa.

Pamoja na kujishughulisha huko, mwisho wa siku lazima arejee nyumbani kujipumzisha bila kujali umbali wake.

Hivyo basi, kwa vyovyote vile lazima uhakikishe nyumbani kunakuwa mahali sahihi, kunakokupa furaha na kunafanyika kuwa nyumbani kwelikweli.

Katika kipindi kama hiki cha mwisho wa mwaka, wengi hupenda kuchukua mapumziko ya kikazi, hivyo ili kutengeneza mwanzo mzuri wa shughuli za kila mwanafamilia kwa mwaka unaofuata ni muhimu kuhakikisha nyumbani panafanyika pa faraja, amani na furaha.

Si tu kwa utulivu, bali panawekwa vizuri kimazingira na kuwapo na mandhari ya kuvutia mtu kupumzika. Zipo njia mbalimbali za kufanya ambazo hazihitaji gharama kubwa ya kifedha ambazo ni rahisi na ni vitu vidogovidogo.

Mojawapo ni mapambo. Ndani ya nyumba yako unaweza kutafuta baadhi ya picha za mapambo ambayo unayapenda na ukapamba.

Tumia pia picha nzuri ziwe za kuchora au zinazoonesha alama ya upendo au yoyote inayokukumbusha enzi au nyakati fulani.

Ipe nyumba yako muonekano na hisia inayotambulisha familia au aina ya watu wanaoishi katika nyumba husika au familia uliyowahi kuwa nayo awali.

Hakikisha muonekano wa nyumba usiwe unaofanana siku zote hususani ndani kuanzia sebuleni, vyumba vya kulala na hata nje kwenye mpangilio wa maua kwa wale wenye nafasi kubwa.

Kila nyumba ina upekee wake na mahitaji tofauti kuendana na wakaaji wake.


Pia usafi ni jambo jingine la kuzingatia ambalo linapaswa kuzingatiwa katika kuweka mazingira yake kuwa ya kuvutia kukaa wakati wote.

Bila kusahau suala la mapishi, ili nyumbani au mtu ajisikie yuko nyumbani lazima kuwe kunapikwa chakula.

Kuna baadhi ya nyumba ambazo hakupikwi ni watu wa kula barabarani tu. Ili nyumba yoyote ile igeuke kuwa nyumbani ni muhimu sana kuwe na chakula, yaani jiko linapotumika kuandaa vyakula na harufu yake nzuri inaifanya kuwa na uhai wa kuitwa nyumbani.

Hata wanaoishi katika nyumba hiyo lazima wajisikie fahari kuishi humo na pia kukumbuka na kupenda kuwapo nyumbani muda wote.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
HIVI HIKI KIJAMAA KINA ROHO NGAPI?
UHALIFU
SASA HIVI TUNAKUJA NA "KATA FUNUA" KUELEKEA 2025
HIZO SI LUGHA ZA MASELA?
KONDA MCHEZO HUO IPO SIKU UTAPOTEZA MENO YA MBELE
BUKU KUMI UNASEMA ETI HUJAPEWA!
TATIZO LAKE KAPOKEA HELA BILA KUTOA TIKETI ILI AJISAHAULISHE
PUSI!
SASA LEO ANGEINUKIA 'ICU'
JAMANI SI NIMERUDISHA CHENJI? KAUSHENI
KULALA MAKABURINI KESI ITAISHA?
ANAJUA MUNGU
KUPATWA KWA WALETI KUBAYA!!!
TABIA HII TANGU LINI?
NIOKOE KWANZA NISIENDE RUMANDE
HIVI WEWE MZIMA KWELI?
NITAKUROGA UWE UNAKATA "UNO" KILA UKILIONA JUA
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...UKISEMA LA MWENZAKO, UWE MSAFI MOYONI MWAKO...

# Jeshi la Israel kubaki eneo muhimu Syria

**TEL AVIV,** ISRAEL

WAZIRI wa Ulinzi wa Israel, Israel Katz amewaagiza wanajeshi wa nchi hiyo kujiandaa kubaki katika eneo huru katika kilele cha Mlima Hermoni wakati wa majira ya baridi.

Eneo hilo muhimu liko kwenye mpaka kati ya nchi za Syria, Lebanon na eneo salama la Umoja wa Mataifa lililoko Milima ya Golan.

Tangazo hilo linawadia baada ya Israel kutwaa udhibiti wa eneo hilo Desemba 8, baada ya kuangushwa kwa utawala wa Rais wa Syria Bashar al-Assad.

Ofisi ya Waziri wa Ulinzi Israel Katz, ilisema katika taarifa yake kuwa kutokana na kile kinachotokea nchini Syria, kuna umuhimu wa kuwepo kwa usalama katika eneo la mlimani.

Katz aliweka picha kwenye mtandao wa X ikimuonesha Waziri Mkuu, Benjamin Netanyahu akiangalia kwa kutumia darubini na kuandika maneno haya, "Ninaangalia kilele cha Syria cha Mlima Hermoni, ambao ulirudi kwa udhibiti wa Israel baada ya miaka 51."

Umoja wa Mataifa umeitaka Israel kujiondoa katika eneo salama, ambalo liko kati ya Syria na Milima ya Golan inayokaliwa na Israel.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa António Guterres alisema katika taarifa yake kwamba inatia wasiwasi na ukiukwaji mkubwa wa maeneo ya Syria.

Umoja wa Mataifa ulisema Israel inakiuka makubaliano ya mwaka 1974 ya kujiondoa kati ya Israel na Syria ambayo yalianzisha eneo salama.

**BBC**



Spika wa Bunge la Korea Kusini, Woo Won Shik, akifungua kikao cha bunge kilichomuondoa madarakani Rais Yoon Suk jana. **PICHA: AFP**

# Hatimaye Rais Yoon Suk kang'olewa madarakani

**SEOUL,** KOREA KUSINI

HATIMAYE Bunge la Korea Kusini limemuondoa madarakani Rais Yoon Suk Yeiol, baada ya jaribio kama hilo kushindikana wiki iliyopita.

Rais Yoon alipigiwa kura ya kutokuwa na Imani na wabunge baada ya kutangaza sheria ya kijeshi iliyodumu kwa muda mfupi na kuleta hofu kwa wananchi.

Katika kikao kilichofanyika jana ambacho kilihudhuriwa na wabunge 300, waliopiga kura ya kumng'oa madarakani, walikuwa 204 na 85 walipiga kura kupinga. Watatu hawakupiga kura, huku kura nane ziliharibika.

Baada ya matokeo kutangazwa, Spika wa Bunge, Woo Won Shik, alisema kuondolewa kwa Yoon madarakani kunatokana na kitendo kilichochochewa na hamu ya wananchi kutaka demokrasia, ujasiri na kujitolea.

Kutokana na kura hiyo, mamlaka na majukumu ya urais Yoon, sasa yamesitishwa na Waziri Mkuu Han Duck-soo atachukua uongozi wake pindi nakala za hati za kuondolewa kwake madarakani zitakapowasilishwa kwa Rais Yoon na Mahakama ya Katiba.

Mahakama ya Katiba ya Korea Kusini ina siku 180 kutoa uamuzi kuhusu mustakabali wa kiongozi huyo ikiwa itamfukuza urais, au atarejeshewa mamlaka yake.

Iwapo ataondolewa madarakani, uchaguzi mkuu utafanyika kumchagua mrithi wake ndani ya siku 60.

Hii ni mara ya pili Bunge kupigia kura hoja ya kuondolewa Rais Yoon. Jumamosi iliyopita alisalimika baada ya wabunge wengi wa chama tawala kususia upigaji kura.

**YOON AJIPA TUMAINI**

Baada ya kura hiyo, Rais Yoon alitoa tarifa akisema hatokata tamaa na amewataka maofisa kudumisha utulivu katika shughuli za kiserikali wakati akijipa matumaini kwamba amesimama kwa muda nafasi ya urais.

"Napokea moyoni mwangu ukosoaji wote, kupewa pole na kutiwa moyo, na uungwaji mkono unaolekezwa kwangu. Nitafanya kila kilicho bora kwa ajili ya nchi yangu hadi dakika ya mwisho," alibainisha Rais Yoon

Hata hivyo, akilihutubia taifa kwa njia ya televisheni baada ya kura hiyo, Rais Yoon alisema ataachia ngazi, lakini hakuomba radhi kutokana na jaribio lake hilo la kutangaza sheria ya kijeshi.

Kiongozi wa chama tawala cha Korea Kusini, Han Donghoon, alisema anachukulia kwa uzito matokeo ya kura hiyo ya bunge ya kumuondoa madarakani Rais Yoon. Hata hivyo kuna kauli za baadhi ya wabunge wa chama hicho kutaka kujiuzulu kutokana na mgawanyiko ndani ya chama.

Lakini, Han alisema ataendelea na majukumu yake.

Waziri Mkuu wa Korea Kusini Han Duck-soo, ambaye sasa anakuwa kaimu rais, ameapa kuhakikisha utawala thabiti.

Han aliahidi atafanya kila awezalo, kuiendesha serikali kwa utulivu, baada ya kura hiyo.

"Moyo wangu ni mzito sana. Ninajitolea kwa nguvu zangu zote na juhudi kuhakikisha kunakuwepo na utawala imara," alisisitiza Han, wakati alipozungumza na waandishi wa habari jana.

Spika wa Bunge Woo Won Shik, ameitaka serikali kushirikiana na kufanya kazi pamoja ili kuleta utulivu wa uchumi na uhusiano wa kigeni.

**MAELFU WAANDAMANA**

Maelfu ya watu waliokusanyika karibu na majengo ya Bunge walishangilia kwa shangwe, huku wakipeperusha mabango.

Katika jiji la Seoul watu waliokuwa na mlengo tofauti wa kisiasa walifanya maandamano ya kumuunga mkono Yoon na wengine waliungana na wabunge kumuondoa madarakani.

Polisi inakadiria kuwa takribani watu 200,000 waliingia kwenye mitaa ya Seoul kuandamana kabla ya kura hiyo kupigwa.

Kwa upande mwingine chama cha upinzani cha Korea Kusini cha Democtatic kimesherehekea na kupongeza hatua hiyo ya bunge ya kumuondoa madarakani Rais Yoon.

"Kura ya leo ni ushindi mkubwa wa watu," alisema Park Cha-dae, kiongozi wa chama hicho.

**UMOJA WA ULAYA**

Wakati huo huo, Umoja wa Ulaya umetoa wito wa kuwepo suluhisho litakalozingatia utaratibu wa amani kutokana na mzozo wa kisiasa unaoendelea nchini humo.

Umoja huo umetoa wito wa kufikiwa azimio la haraka katika kumaliza mzozo huo.

Msemaji wa Umoja wa Ulaya Anitta Hipper, alisema katika taarifa yake kuwa umoja huo unauzingatia uamuzi wa Bunge la Taifa la Korea Kusini la kumuondoa madarakani Rais Yoon.

"Ni muhimu sasa kuhakikisha utatuzi wa haraka unapatikana na wenye kuzingatia utaratibu katika mzozo wa kisiasa, kulingana na katiba ya Korea," alifafanua Hipper.

**DW**

# Majaliwa asisitiza serikali kuweka mazingira rafiki kuvutia uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa (pichani), ametembelea kiwanda cha kutengeneza dawa za binadamu cha CURE AFYA kilichoko Kigamboni, Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya kushuhudia uzalishaji wa dawa kwenye kiwanda hicho chenye thamani ya takribani Sh. bilioni 50, Waziri Mkuu alisema serikali itaendelea kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji ili kuhakikisha wawekezaji wanapata faida kutokana na shughuli zao.

Majaliwa pia alitoa wito kwa wawekezaji hao kuendelea kutengeneza dawa zilizo katika ubora unaokubalika katika viwango vya kimataifa kwenye utoaji wa huduma za tiba.

"Serikali imefanya uwekezaji mkubwa kwenye ujenzi wa miundombinu ya utoleaji huduma za afya nchini, na sasa tunahitaji kupata dawa na vifaa tiba kwa ajili ya kuendelea kuongeza nguvu kwenye utoaji huduma, hivyo uwekezaji huu una tija kwa taifa letu," alisema.

Pia aliwataka watumishi wa kiwanda hicho kufanya kazi kwa uaminifu, uadilifu na weledi ili kumsaidia mwekezaji huyo kupata faida kutokana na uwekezaji wake.

Katika hatua nyingine, Majaliwa ametembelea eneo la Dege, Kigamboni mkoani kukagua utekelezaji wa agizo alilolitoa la uwekaji wa taa za Barabarani wakati wa ziara yake aliyoifanya wilayani humo Oktoba, mwaka huu.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa agizo hilo Mkurugenzi wa Halmashauri ya manispaaa Kigamboni, Erasto Kiwale, alisema mpaka sasa taa 67 zimeshawekwa katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo na kazi inaendelea.



# Maofisa watendaji waonywa kuhusu upendeleo

**Na Mwandishi Wetu**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma, Elizabeth Gumbo, amewaonya maofisa watendaji wa kata na vijiji kuhusu upendeleo katika mchakato wa kuwapata wahudumu wa afya ngazi ya jamii.

Gumbo alitoa onyo hilo jana katika ufunguzi wa Mafunzo Elekezi ya Mpango Jumuishi wa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii kwa maofisa watendaji wa kata 16 , wa vijiji 56 na wasimamizi wa vituo vya huduma za afya 45 wa halmashauri hiyo yaliyofanyika Shule ya Sekondari Maposeni katika Ukumbi wa Mikutano wa Jenista Joakim Mhagama.

"Mhudumu wa afya ngazi ya jamii anayeomba yeye maombi ndiye anayefanya kwa ufanisi, Watendaji wa Kata na vijiji acheni upendeleo kwa kuleta watu wenu," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema wahudumu wa afya ngazi ya jamii wana mchango mkubwa katika jamii.

"Wahudumu wa afya ngazi ya jamii ni muhimu kwa sababu wao ndio kiungo cha serikali na jamii na wanarahisisha kufikisha elimu ya afya haraka, mfano elimu ya lishe na chanjo na wanaongea lugha moja na wananchi kwani wanatoka kwenye maeneo ya jamii husika," alisema.

Rajab Tamimu, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Parangu ambaye pia ni Mwenyekiti wa Maofisa Watendaji wa Kata katika Halmashauri ya Songea na Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Peramiho B, Rehema Nombo, walisema mafunzo hayo yatawarahisishia usimamizi uchaguzi wa wahudumu wa afya ngazi ya jamii huku wakipongeza serikali kwa kuja na Mpango Jumuishi wa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii katika mkoa wa Ruvuma.

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Mke wa mtu ni sumu



**Na Adam Fungamwango**

KUMPENDA mke wa rafiki yako kweli ni hatari, viko vitu vya kupenda lakini vingine vina madhara, oooh moyo utakupeleka kaburini."

Hicho ni kiitikio cha wimbo uitwao, 'Ushinde Moyo Wako', uliopigwa na OTTU Jazz, wana wa Msondo Ngoma, utunzi wake marehemu, Tx Moshi William.

Wimbo huu ulirekodiwa mwanzoni mwa miaka ya 1990, lakini maana na maudhui yake yataishi milele, daima hadi mwisho wa dunia hii.

Unawaasa watu wenye tabia ya kupenda au kutongoza wake za watu.

Wengine wanakwenda mbali zaidi wanawachukua mpaka wake za rafiki zao.

Kama Tx Moshi alivyobainisha hapo kuwa kitu hicho ni cha hatari kwa sababu inawezekana kabisa kinaweza kumpeleka mtu kaburini.

Ndiyo maana wako waliobainisha kuwa mke wa mtu ni sumu. Maana yake mwenyewe akigundua anaweza kufanya chochote kinachoweza kuhatarisha maisha yake mwenyewe, mkewe au yule aliyefanya kitendo hicho.

Na kitu kama hicho hakiwezi kutafsiriwa vyovyote vile zaidi ya tamaa na ugomvi, kwani wanawake waliojaa katika dunia hii ya Mungu leo kwenda kuchukua mwanamke ambaye ameolewa tayari au mke wa mtu unayemfahamu?

Vitu kama hivi vimetokea sana kwenye jamii na tumeshuhudia kusababisha matatizo makubwa kwa wahusika na hata jamii kwa ujumla.

Kwanza kabisa, mwenyewe akijua anaweza kuchukua uamuzi wa kujimaliza mwenyewe. Wapo ambao hawana uvumilivu hata chembe, wao wanaamua kujidhuru.

Wengine hawana tabu, wao wanatoa talaka tu. Unaweza ukadhani labda hii ni afadhali kwa sababu kunakuwa hakuna maafa, lakini athari zake ni kwamba mume na mke wanaachana kwa sababu ya mpuuzi fulani, mwanamke anahangaika kwa sababu amedanganya na kutelekezwa, lakini pia kama wana watoto pia wanaanza kuteseka kwa kukosa malezi mema.

Mbaya zaidi kule wale wenye visasi. Asipomfanyizia mkewe, atafanya kila njia kumfanyizia yeyote aliyefanya kitendo hicho kwa mkewe.

Tumeshuhudia watu wakifanyiwa vitendo vibaya, wengine wakitekwa, wapo wanaouawa na hii yote ni kwa sababu ya visasi vinavyosababishwa na mambo hayo.

Waswahili wana msemo wao, 'cheza na mtu, usicheze na mke wa mtu.' Hawatanii, wanamaanisha kweli.

Ukisoma mashairi ya wimbo wa Msondo unaonya kila kitu, unaweza kupitia hapa.

"Usiendekeze ee moyo utakavyokutuma. Unadanganya jaribu kushinda, usiposhinda, huna budi kuumia, utajivisha kitanzi pasipo huruma.

"Kumpenda mke wa rafiki yako kweli ni hatari, viko vitu vya kupenda lakini vingine vina madhara, oooh moyo utakupeleka kaburini.

Nakuomba jirekebishe bwana, tabia hiyo siyo nzuri bwana, ni kitendo cha aibu na kashfa ya hali ya juu, tunakusihi sana acha mara moja.

Ulijua huyo ni ndugu yako na rafiki yako swahiba na leo wamsaliti, vipi sasa wanamtamani shemejiyo? Sikio la kufa halisikii dawa."

Hata mwanamuziki Marijani Rajab hakukaa kimya kwenye hili. Miaka ya 1980 alitunga wimbo aliouita 'Mwana Umepotea,' ambao una mashairi haya.

"Mzee Said ee alikuja lalamika ee, kasikia fununu kwamba unavuruga nyumba za watu kaja kutoa onyo anasema kijana ole wako, nasikitika sana ndugu yangu kuwa na mambo hayo, umefanya mambo mengi lakini haya yamezidi kipimo, mchezo na nyumba za watu sawa sawa kucheza na moto. Wacha wacha mara moja, hatari kubwa. Utapoteza maisha baba, na wewe ungali mdogo, hujaiona dunia baba, chonde chonde nakuomba baba."

Kaka anamwambia mdogo wake kuwa mjumbe mzee Said alikwenda nyumbani kwao kulalamika juu ya tabia ya kijana huyo kucheza na nyumba za watu. Maana yake anachukua wake za watu. Marijani akamuasa kuwa tabia hiyo ni sawa na kucheza na moto, matokeo yake atapoteza maisha wakati bado ni kijana mdogo.

Huyu ni kijana wa mwisho aliyedekezwa kiasi kwamba tabia yake ikawa mbaya, akawa anafanya kila kitu kibaya mama wizi na mambo mengine kama ulevi, huku akikingiwa kifua na mama yao. Matokeo yake sasa akajiingiza kwenye janga la kutamani wake za watu.

"Ewe kipenzi cha mama ee, ewe ndugu yetu kitinda mimba, hebu tizama unavyofanya kwanza. Mbona nakuona unapotea, mama naye mapenzi kazidisha kwako, hata kukukanya anashindwa, anakuacha ufanye unavyotaka mwana.

Sasa imebidi nikueleze, nakwambia kama mimi ni kaka yako, ingawa natambua unanidharau, lakini mimi ndiyo nimeona dunia mwanzo." Hicho ni kipande cha kwanza wimbo huo. Narudia, mke wa mtu ni sumu.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

# Nyuma ya Pazia-13

TAARIFA za habari kwenye televisheni, redio, mitandao ya kijamii zinaarifu kutekwa kwa mtoto wa miaka sita, Macaire, mwanafunzi wa darasa la kwanza katika shule moja Mbezi Dar es Salaam. Mashuhuda wanasema alinyakuliwa na mwanamume mmoja aliyeshiba, kujaa misuli na kukimbilia kwenye gari lililokuwa pembeni mwa barabara ya Bagamoyo, Dar es salaam, ambalo mlango wake ulikuwa wazi. Wazazi wa mtoto wanapigiwa simu na watekaji wakitaka kiasi cha Sh. Milioni 15 ili wamwachie. Jeshi la Polisi linaingia kazini kumsaka au kuwasaka watekaji. Walichogundua ni kisa cha kushangaza, kusisimua ambacho utakipata utakaposoma kila aina ya nakala ya gazeti hili, ili kuupata mkasa mzima wa tukio.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

TAYARI Dora alionekana kumzoea Eddy na hii ni kwa sababu mpelelezi huyo ni mtu wa utani na kuzoeleka kwa urahisi. Pia hakujua kama ni mpelelezi, ila mwandishi wa habari, kazi ambayo ndiyo alijitambulisha nayo.

"Nipe habari shemeji. Nadhani umefanya kazi nzuri." "We acha tu, haikuwa rahisi ndugu yangu, mbishi yule baba!" "Enhe ulipofika ulimfanya nini hadi akakubali na amesema kama amewasiliana na watekaji?" Akauliza na kumuacha kwanza akae kwenye kochi la ofisini.

"Mwenzako nilipotoka hapa nikampigia simu tukutane kwa ajili ya kutafakari jambo hili kwa sababu mtoto ni wangu mimi na yeye.

Akawa mgumu, lakini nimemdanganya kuwa nina wazo ambalo linaweza kusababisha mtoto apatikane kwa haraka.

Akaniuliza tukutane wapi, maana kwake hataki, mchumba wake anaweza kufika muda wowote. Nikamwambia tukutane faragha, kwenye hoteli yoyote kwa sababu wote wawili tuna mahusiano, hakuna yeyote anayetaka kuyavunja. Akaniambia niende kwenye hoteli ya Malimba kule Sinza.

Nikaenda tukakutana. Ilikuwa ndani tukaongea, nikamdanganya. Mimi mtoto wa kike bwana, nikamlegeza pale akalegea mwenyewe.

Baada ya kumaliza nikamuuliza, enhee walikupigia simu watekaji, wanasemaje? na wapi safari hii?"

"Wamemwambia apeleke maeneo ya Kigamboni, kesho, awe amefika pale saa nne usiku." "Kigamboni kubwa mama, sehemu gani?"

"Amesema ni katikati ya msitu mdogo utokao Kibada kwenda Tuangoma.

Upande wa kulia kama unakwenda Tuangoma kuna ujenzi wa kiwanda unaoendelea.

Mwisho wa uzio wa kiwanda hicho kwa mbele, ndipo pesa hizo zinatakiwa kuwekwa.

Na wamesema iwe saa nne usiku kwa sababu ni msitu hivi." Akajibu Dora.

Eddy akitikisa kichwa na kumuuliza kimzaha, "ni kweli au alikuwa akikudanganya ili apate kile alichokosa kwa miaka mingi?"

"Ni uhakika kabisa, na nadhani safari hii askari polisi hawashirikishwi kama wewe ulivyosema basi sidhani kama itashindikana na mtoto atapatikana kama inavyokuwa mara kwa mara."




"Mtoto atapatikanaje?" "Hilo hakuniambia, lakini najua kama watekaji wakipata hizo pesa mtoto atapatikana tu kwa sababu lengo lao wao ni pesa tu na si kitu kingine." "Okay, basi sawa."

**Wakazungumza muda mrefu kidogo, baada ya hapo wakaagana. Kitu ambacho kilikuwa kichwani mwa Eddy ni kwamba Jeshi la Polisi kwa sasa halijui chochote juu ya mpango huu wa sasa wa kuwapelekea watekaji pesa.**

Wakazungumza muda mrefu kidogo, baada ya hapo wakaagana. Kitu ambacho kilikuwa kichwani mwa Eddy ni kwamba Jeshi la Polisi kwa sasa halijui chochote juu ya mpango huu wa sasa wa kuwapelekea watekaji pesa.

Wanaofahamu ni wazazi wawili tu. Macky na Dora. Pia wote wawili wanafahamu kuwa safari hii askari polisi hawajihusishi kabisa na tukio hili. Kwa sababu kila mmoja anajua pesa haijatoka polisi bali kwa raia ambaye ni mwandishi wa habari.

Alijua mtego alioweka kwa kiasi kikubwa unaweza kufanikiwa. Ila kitu kimoja alichokuwa na wasiwasi nacho ni Macky kutokuwa na siri kumwambia mzazi mwenzake.

Tena alichosema Dora ni kile kile kama alichoambiwa na Macky.

Ina maana ni kweli kabisa Dora amekutana na mzazi mwenzake, wameongea ya kuongea na kumpa siri hiyo.

Hicho ndicho alichokuwa na wasiwasi nacho, kwani hajui sasa nani anaweza kuiingilia siri hii na kuvujisha kwa askari polisi, ingawa wote wawili wameshaonya juu ya hilo.

************************************

Hakutaka kabisa kuchukua gari yake siku hiyo. Alitaka kwenda kwa kutumia basi kama mtu mwingine wa kawaida tu.

Alichukua redio yake ndogo ambayo ni kinasa sauti. Kalamu na kijitabu kidogo kama mwandishi wa habari.

Tochi ndogo, kamba imara, kisu kidogo, na bastola ya kawaida, lakini imetengenezwa maalum kuzuia sauti, pamoja na nyingine ya akiba inayofanana na kalamu.

Nayo vile vile haitoi sauti. Alichukua pia kichupa kidogo ambacho kina aina fulani ya poda ambayo ni sumu.

Sumu isiyoua, ili kumfanya binadamu apoteze fahamu kwa siku tatu au nne hivi.

Kama ni mtu ambaye afya yake mgogoro angeweza kuzirai kwa siku tatu.

Alipanda daladala kutoka nyumbani kwake maeneo ya Victoria, Dar es Salaam na kwenda hadi Kivukoni.

Alipanda moja ya pantoni zilizokuwa Feri hadi ng'ambo, Kigamboni. Ilikuwa saa moja usiku muda huo. Kama kawaida ya wapelelezi.

Kwenye eneo la tukio huwahi au kuchelewa. Huwa hawaendi kwa wakati ambao umepangwa, au kupangiana na mtu, au aliuopanga mwenyewe.

Siku zote huamini kuwa ukienda kwenye wakati mwafaka ni kujipeleka mwenyewe kwenye mkono wa adui au mdomoni mwa kifo.

Huamini kuwahi kusoma mazingira ya wito au kitu ambacho anakifuata kama kiko salama, mtego, au kuwapata anaowahisi kirahisi zaidi. Kuchelewa pia hufanya kama kulikuwa na mpango wa kumalizwa au kukamatwa, basi kuwafanya maadui kuhamanika na kuwa rahisi kufahamu mipango yao kama utakuwa makini na kachero mzoefu.

Alipofika alipanda daladala inayoelekea maeneo ya Tuangoma. Ilikuwa ni safari ndefu kidogo.

Alifika Mikadi, Mjimwema, Kibada, Maliasili na alishuka kituo cha mbele.

Hakukuwa na taa nyingi, kwani halikuwa eneo la makazi ya watu. Badala yake ni viwanda vikubwa vilivyojengwa kando ya barabara. Yeyote yule angeweza kuogopa, lakini kwa upande wa Eddy alipenda mazingira hayo.

Aliona yatamrahisishia kazi na kuifanya kwa utulivu na uhakika na kiwango cha hali ya juu.

Alisogea hadi eneo ambalo aliambiwa kuwa ndiyo sehemu ya tukio.

Alivuka barabara kwenda upande wa pili ambao hata kama kungekuwa na mtu au watu wanaomtazama wasingemtilia shaka.

Alionekana kama anapita eneo hilo bila wasiwasi wala kuonekana kama kuna kitu anahisi.

Alikwenda mbele kidogo, eneo ambalo barabara imeinuka kidogo, yaani mlima na kona kali.

Alipopita hapo alikata barabara isiyokuwa na lami iliyokuwa upande wa kushoto.

Akavuka tena barabara kuu ya kwenda Tuangoma, akaingia kwenye barabara nyingine ya vumbi. Alienda nayo hadi alipohisi kuwa akikata kona upande mwingine na kushoto na kuambaa pori kwa pori anaweza kufika eneo lililotajwa na Macky kwa usahihi, bila kujulikana na mtu yeyote.

Alijua kabisa kuwa anakopita hawezi mtu yeyote ambaye hana shughuli maalum kupita pale. Aliambaa kwenye pori hilo dogo taratibu kwa dakika kama tano hivi.

Alihisi kuwa mbele kuna jengo. Ni lile lile ambalo aliambiwa na Macky.

Hapo aliinama chini na kuanza kutambaa ili kutomshtua yeyote ambaye atakuwa anakaribia hapo au kuwapo.

Aliangalia saa yake ilitimu saa mbili na nusu usiku.

Ni muda ambao alijua watekaji watakuwa tayari wameshafika kama watakuwa hawajapata taarifa nyingine ya kuwatishia au kuwatonya.

**Itaendelea Jumapili**



# WAHITIMU NAFASI ACADEMY KUFANYA MAONESHO

KITUO cha kuendeleza sanaa jijini Dar es Salaam, Nafasi Art Space, kimefanya maonesho kwa ajili ya wasanii waliohitimu mafunzo.

Uongozi wa kituo hicho ulisema wasanii hao walifanya maonesho mbalimbali kama kuhitimisha safari ya mafunzo ya miezi 11 ambayo yamewaongezea hamasa,mabadiliko na nguvu ya kujielezea kisanii.

Uongozi wa kituo hicho umewaomba wadau wa sanaa kuungana na wahitimu hao katika safari yao ambayo watakabiliana na changamoto mbalimbali.



# MBILIA BEL KUWASHA MOTO BIBI TITI MEMORIAL FEASTIVAL

MWANAMUZIKI Mkongwe kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Mbilia Bel, amesema wananchi watakaohudhuria tamasha la Bibi Titi Memorial, atawapa burudani ya aina yake na itakuwa kumbukumbu kwao.

Akizungumza mara baada ya kutua nchini, msanii huyo amesema amefurahi kuja tena nchini, na kutokana na mapenzi waliyoyaonesha Watanzania, kazi itakuwa kwake kuwafurahisha kwa kuimba nyimbo zake zote maarufu.

Tamasha la Bibi Titi Memorial ambalo linafanyika Ikwiriri Rufiji Mkoa wa Pwani lilianza Desemba 12 na linamalizika leo kwa wasanii mbalimbali kutoa burudani kwa watu watakaohudhuria.

Mbunge wa jimbo la Rufiji ,Mohammed Mchengerwa alisema dhamira ya Tamasha hilo ni kuwaunganisha Waafrika wote kama alivyokuwa Bibi Titi ambaye alipendwa na kuaminika na watu wa Afrika nzima.

## ZISIKUPITE

### CITY YAMTAKA WRTZ, BRUNO

KIUNGO wa kati wa Bayer Leverkusen na Ujerumani, Florian Wirtz, mwenye umri wa miaka 21, na kiungo wa kati wa Newcastle United, Bruno Guimaraes (27), wanafuatiliwa na Manchester City. **(Times)**

### ZUBIMENDI ATAJWA CITY

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola pia atapata uungwaji mkono kumsajili kiungo wa kati wa Real Sociedad na Timu ya Taifa ya Hispania, Martin Zubimendi, mwenye umri wa miaka 25. **(ESPN)**

### CHELSEA, LIVERPOOL VITANI

CHELSEA na Liverpool zinatazamiwa kumwinda mlinzi, Milos Kerkez, mwenye umri wa miaka 21, lakini Bournemouth watafanya kila wawezalo kuhakikisha wanambakisha mchezaji huyo wa kimataifa wa Serbia. **(Football Insider)**

### VLAHOVIC ANUKIA ARSENAL

MIKEL Arteta anataka kumwongeza mlinzi wa Juventus na Timu ya Taifa ya Serbia, Dusan Vlahovic, mwenye umri wa miaka 24, kwenye kikosi chake cha Arsenal ifikapo Januari. **(Caught Offside)**

### HERNANDEZ NJIA MOJA

REAL Madrid imejindoa kwenye kinyang'anyiro cha kumsajili mlinzi wa AC Milan, Theo Hernandez, mwenye umri wa miaka 27 na kurahisisha kazi kwa Manchester United wanaomtaka mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa. **(Fichajes)**

### IRAOLA SOKONI ENGLAND

KLABU ya Bournemouth inataka Kocha, Andoni Iraola, atie saini mkataba mpya kutokana na hofu klabu nyingine za Ligi Kuu England zinaweza kumlenga Mhispania huyo. **(TBR Football)**

### RB KUMBANA SIMONS

KLABU ya RB Leipzig inataka kumsajili mshambuliaji wa Uholanzi na Paris St-Germain, Xavi Simons, mwenye umeri wa miaka 21 kwa mkataba wa kudumu, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa Liverpool. **(Caught Offside)**

### LEON AKARIBIA UNITED

KLABU ya Manchester United imefikia makubaliano ya mdomo na Cerro Porteno ili kumnunua beki wa pembeni wa Paraguay, Diego Leon, mwenye umri wa miaka 17. **(Fabrizio Romano)**

### UNITED KUMUUZA ERIKSEN

KIUNGO wa kati wa Denmark, Christian Eriksen, mwenye umri wa miaka 32, anaweza kuuzwa na Manchester United katika dirisha la Januari endapo itatolewa ofa ya kuvutia. **(Florian Plettenberg)**

### NUAMAH ATAJWA EVERTON

KLABU ya Everton inapanga kumnunua winga wa Lyon na Timu ya Taifa ya Ghana, Ernest Nuamah, mwenye umrei wa miaka 21 ifikapo Januari. **(Football Insider)**

### FRIEDKIN KUINASA EVERTON

KUNDI linaloongozwa na Dan Friedkin linakaribia kufikia makubaliano ya kuinunua Everton, na mchakato wa ununuzi ukitajwa unaweza kukamilika wiki ijayo. **(Times)**

### SPURS YAMKANA WERNER

KLABU ya Tottenham Hotspur haina mpango wa kuchagua kumsajili mkataba wa kudumu mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Timo Werner, mwenye umri wa miaka 28, kutoka RB Leipzig mwishoni mwa msimu huu. **(GiveMeSport)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MESSI AFUNGUKA UBORA WA YAMAL

## ●●● Asema chipukizi huyo wa Hispania anamkumbusha 'udogo' wake...

**HERZOGENAURACH,** Ujerumani

LIONEL Messi amekiri nyota aliyechipukia wa Barcelona, Lamine Yamal, humkumbusha yeye mwenyewe wakati alipokuwa mdogo.

**Messi aliulizwa mapema wiki hii wakati wa hafla katika makao makuu ya Adidas ya Herzogenaurach nchini Ujerumani na msanii wa Nigeria, Goke Oyewo, kumtaja mchezaji wa kizazi kipya aliyemkumbusha alipokuwa mdogo.**

"Kuna kizazi kizuri sana cha wanasoka wachanga ambao wana miaka mingi mbele yao," alisema Messi.

"Ikiwa nitachagua mtu, kwa sababu ya umri na kwa sababu ya siku zijazo alizonazo, nimesikia wamemchagua, Lamine Yamal na bila shaka ni yeye kwa ajili yangu pia.

"Nakubali inategemea yeye na mambo mengi kwa sababu ndivyo soka lilivyo, lakini yeye ni wa sasa na bila shaka ana mustakabali mkubwa."

Yamal ni zao la akademi ya vijana ya Barcelona ya La Masia ambako pia Messi alipitia.

Mshindi huyo mara nane wa tuzo ya Ballon d'Or, Messi, mwenye umri wa miaka 37, aliondoka Barca mwaka 2021 baada ya kushinda rekodi ya mataji 34 ndani ya miaka 21 kwenye klabu hiyo.

Yamal mwenye umri wa miaka 17, alitajwa mchezaji bora chipukizi wa Euro 2024 baada ya kuisaidia Hispania kubeba taji hilo, na alimaliza katika nafasi ya nane kwenye tuzo za Ballon d'Or.

Fowadi huyo wa Hispania amefunga mabao matano na kutengeneza mengine 10 katika mechi 15 za ligi msimu huu na kuisaidia Barca kuongoza msimamo wa LaLiga.

"Ningependa kuona Barca ikishinda LaLiga, Copa del Rey na pia Ligi ya Mabingwa Ulaya," alisema Messi.

# MBAPPE KUSAFIRI NA MADRID QATAR



**MADRID,** Hispania

KYLIAN Mbappé ameukosa mchezo mmoja wa Ligi Kuu Hispania kutokana na jeraha la mguu, lakini Kocha wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, anatumaini mshambuliaji wake huyo atapona kwa wakati ili kucheza fainali ya Kombe la Mabara (Klabu Bingwa ya Dunia) wiki ijayo.

Kombe la Mabara limeboreshwa sasa likiitwa Klabu Bingwa ya Dunia, na kuanzia mwakani litakuwa na timu 32.

Ancelotti alisema jeraha la paja la mguu wa kushoto ambalo Mbappe alipata wiki hii lilimfanya kuwa nje ya mechi ya LaLiga huko Rayo Vallecano iliyochezwa jana.

Lakini kocha huyo raia wa Italia alisema Mbappé atasafiri na wachezaji wenzake hadi Qatar kwa fainali ya Kombe la Mabara itakayochezwa Desemba 18, mwaka huu wakati Madrid itamenyana na Pachuca au Al Ahly.

"Tutaona kama anaweza kucheza bila kuchukua hatari yoyote (ya kuumia)," alisema Ancelotti akiwaambia waandishi wa habari. "Atasafiri kwa sababu tunadhani anaweza kupona jeraha hilo."

Mbappé aliumia mguu na akatolewa baada ya kufunga bao lake la 50 la Ligi ya Mabingwa Ulaya katika ushindi wa magoli 3-2 wa Madrid dhidi ya Atalanta uliofanyika Jumanne iliyopita.

"Ni vigumu kusema [majeraha] yanatoka wapi," Ancelotti aliongeza.

"Katika mapumziko mawili ya mwisho ya kimataifa amekuwa hapa akifanya kazi nasi, ameimarika, nashukuru ni kipindi kidogo ambacho atakuwa nje, sidhani kama atapoteza kile alichoweza kuzalisha katika michezo michache iliyopita. ."

Ancelotti alithibitisha kiungo wa kati wa Ufaransa, Eduardo Camavinga, yuko tayari baada ya kupona tatizo la misuli ya paja huku beki wa Austria, David Alaba akikaribia kurejea kutokana na jeraha la goti.

# Slot aitaja timu ngumu EPL 2024/25

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Arne Slot, amekiri hakuna timu msimu huu ambayo imeipa timu yake mtihani mgumu kama Chelsea, na akasisitiza walipokutana Oktoba walikuwa kwenye wakati mgumu mno.

Kikosi cha Slot kiko pointi nne mbele ya timu hiyo ya London Magharibi kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu England kikiwa na mchezo mmoja mkononi, huku sehemu kubwa ya faida hiyo ikipatikana katika ushindi mgumu wa 2-1 dhidi ya Chelsea kwenye Uwanja wa Anfield.

Licha ya hali ya sasa ya Chelsea kama mpinzani wa karibu zaidi wa Liverpool, Kocha, Enzo Maresca, amesisitiza mara kwa mara timu yake haiko tayari kushindania taji la Ligi Kuu.

Lakini Slot amesema katika mbio za ubingwa msimu huu Chelsea haipaswi kupuuzwa.

"Ilikuwa moja ya michezo, labda mchezo pekee, ambapo nilihisi timu nyingine ilikuwa bora kuliko sisi wakati wa mchezo huo," alisema Slot kuhusu pambano lao la Oktoba dhidi ya Chelsea.

"Hiyo haisemi kwa muda mrefu wao ni bora kuliko sisi, lakini wakati wa mchezo walikuwa na uwezo mkubwa wa kumiliki mpira kuliko sisi na walikuwa walitutisha kuliko timu nyingine yoyote hadi sasa.

"Sipo hapo kuhukumu ni nafasi gani watamaliza kwenye jedwali la ligi. Ni lazima niangalie timu yangu, lakini Chelsea imekuwa ya kuvutia msimu huu hadi sasa, hilo ni la uhakika."

Maresca amekuwa akisisitiza mara kwa mara vijana wake wa Chelsea hawako tayari kushindana na Liverpool, Manchester City na Arsenal kwa sababu ya kutokuwa na uzoefu wa kucheza mechi kubwa.



# Tuchel amsubiria Palmer England



**LONDON,** England

KOCHA ajaye kwa Timu ya Taifa ya England, Thomas Tuchel, amekiri furaha yake ya kufanya kazi na nyota wa Chelsea, Cole Palmer.

Palmer aliibuka kama nyota wa Ligi Kuu England msimu uliopita na kumfanya kocha wa zamani wa England, Gareth Southgate kumchukua kwenye michuano ya Euro 2024, ambapo alisaidia timu kutinga nusu fainali na alifunga kwenye mechi ya fainali.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 anaendelea kung'ara katika ngazi ya klabu akiwa na Chelsea na Tuchel aliombwa kufahamu mipango yake kwa nyota huyo wa The Blues.

"Hiyo ni mbali sana, kwenda kwa wachezaji binafsi!" alisema Tuchel akiiambia Sky Sports News.

"Lakini kwa hakika yuko kwenye kiwango, nadhani kila mtu angekubaliana na hilo.

"Tunatumaini bado anaweza kukua na kuweka kiwango chake. Kila mtu anafurahia kumtazama. Yeye ni mtulivu, ni mzuri sana katika kumalizia na kusaidia. Inavutia sana kwa sasa."

Tuchel anapanga kuhudhuria mechi kadhaa za Ligi Kuu ya England katika mwaka mpya ili kumtazama kwa karibu Palmer na wachezaji wengine wanaopigania nafasi katika kikosi cha England.

"Mtaniona viwanjani kuanzia Januari," aliongeza Tuchel.

# KOCHA AZAM FC AKUBALI UBORA TABORA UNITED

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Azam FC, Rachid Taoussi, amekiri Tabora United ilikuwa na haki ya kushinda dhidi ya kikosi chake kutokana na aina yao ya uchezaji na kuongeza timu hiyo inaweza kutumia kwa usahihi makosa ya wapinzani wao.

Tabora United imeichapa Azam FC mabao 2-1 katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani, Tabora juzi.

Taoussi alisema katika soka timu haishindi kwa ufundi na mifumo tu peke yake, bali kupambana, kujituma na kuwa makini muda wote.

"Tabora United ni timu nzuri sana, naifahamu, nimeshawahi kuona mechi zake kadhaa huko nyuma, ni timu inayoweza kutumia kwa usahihi makosa ya wapinzani, ukifanya kosa wanakuadhibu, tumefanya makosa mawili yaliyotugharimu.

Katika mpira mnaweza kucheza kwa ufundi na mifumo, lakini ndani ya uwanja siyo hivyo tu vinaweza kuwapa ushindi, inabidi pia muwe na nguvu, kupambana, kujituma, kutotengeneza makosa yasiyo ya lazima, pia na kuwa makini muda muda wote, inawezekana pia uwanja haikuwa rafiki kwetu, lakini tunakubali tumeshindwa katika mchezo wa leo ni lazima tuheshimu hilo," alisema kocha huyo raia wa Morocco.

Naye Kocha Mkuu wa Tabora United, Anicet Makiadi, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DR Congo), ambaye ameonekana kuibadilisha timu hiyo na kuwa moja ya timu tishio alisema siri ya ushindi ni kufanya mazoezi kwa bidii tu na si kitu kingine.

"Tunafanya kazi kwa bidii, kufanya mazoezi, wachezaji wanafuata kile ambacho nawafundisha, wana nidhamu ndani na nje ya uwanja, ndicho kinawapa Tabora United hiki wanachokipata sasa," alisema kocha huyo.

Mabao ya Tabora United katika mechi hiyo yaliwekwa wavuni na Heritier Makambo dakika ya 37, kabla ya bao la kujifunga la kipa, Muhamed Mustafa, dakika ya 68, huku lile la kufutia machozi la Azam likifungwa na beki wa kati, Yoro Diaby dakika ya 71.

Hata hivyo licha ya kufungwa, Azam bado inaendelea kukaa kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na pointi 30 huku Tabora United ikipanda hadi nafasi ya tano baada ya kufikisha pointi 24.




Mchezaji wa Timu ya Magongo ya Kinyerezi, Amina Omary (katikati), akiwania mpira dhidi ya nyota wa Buza katika mashindano ya JMK Park yaliyofanyika kwenye Kituo cha Michezo cha Jakaya Mrisho Kikwete jijini, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Serengeti Boys kibaruani Uganda

**Na Somoe Ng'itu**

TIMU ya Soka ya Taifa ya vijana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Boys), inatarajia kukutana na wenyeji Uganda katika mechi ya kwanza ya kuwania tiketi ya kufuzu Fainali za Kombe la Mataifa Afrika (AFCON U-17), itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Nakivubo jijini Kampala.

Kocha Mkuu wa Serengeti Boys, Boniface Pawasa, amesema kikosi chake kiko tayari kwa ajili ya mchezo huo na wamejiandaa kukutana na ushindani kutoka kwa wapinzani wao.

Pawasa alisema hakuna mechi rahisi katika mashindano hayo yanayoshirikisha nchi sita na wataingia kucheza kwa nguvu na tahadhari.

Beki huyo wa zamani wa Simba na Taifa Stars, alisema wamejipanga kutetea ubingwa na michuano hiyo ili kuendeleza rekodi nzuri ya kushiriki fainali za Afrika mfululizo.

"Tunafahamu mashindano ni magumu lakini maandalizi tuliyofanya yanatupa mwanga wa kufanya vizurim tumekuja kupeperusha vyema bendera ya Tanzania. Tunajua kila timu inahitaji kufuzu AFCON, haitakuwa michuano ya kusindikiza, kila mchezo ni vita," alisema Pawasa.

Serengeti Boys iliyoko Kundi A itashuka tena uwanjani Desemba 18, mwaka huu kukutana na Kenya na timu mbili zitakazofanya vizuri kutoka kila kundi zitatinga hatua ya nusu fainali itakayochezwa Desemba 24, mwaka huu.

Kundi B la mashindano hayo linaundwa na Somalia, Sudan na Sudan Kusini wakati fainali za mashindano hayo zimepangwa kufanyika Desemba 27, mwaka huu.

# Fountani Gate FC hesabu kali Ligi Kuu Bara

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kupata ushindi, benchi la ufundi la Fountain Gate FC, limesema kwa sasa linaelekeza nguvu zake kuelekea mchezo unaofuata ambao utachezwa keshokutwa dhidi ya wenyeji Azam FC.

Kocha Mkuu wa Fountain Gate, Mohamed Muya, alisema baada ya kupata pointi tatu katika mchezo wao uliopita wanajipanga kuendelea kupata ushindi mfululizo.

"Kwa sasa tunaelekeza nguvu zetu katika mchezo ujao dhidi ya Azam FC, ni mchezo ambao tunatarajia utakuwa mgumu na wenye ushindani, kwa sababu hiyo tunapaswa kufanya maandalizi mazuri na mapema, " alisema Muya.

Kocha huyo alisema amefurahishwa na viwango vilivyoonyeshwa na wachezaji wake katika mchezo uliopita dhidi ya Coastal Union ambapo walipata ushindi wa mabao 3-2.

"Tumepata ushindi mnono kutokana na juhudi iliyofanywa na wachezaji wangu, ushindi huu umenipa matumaini makubwa, kikubwa walifuata maelekezo ya ndani na nje ya uwanja," kocha huyo aliongeza.

# Yanga Princess, JKT Queens keshokutwa

**Na Somoe Ng'itu**

MECHI ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania kati ya Yanga Princess dhidi ya JKT Queens sasa itachezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa KMC, Dar es Salaam, imeethibitishwa.

Kwa mujibu wa ratiba mpya ya ligi hiyo iliyotolewa juzi jijini, ligi hiyo itaendelea tena Desemba 21, mwaka huu kwa Mashujaa Queens kuwavaa Simba Queens wakati Ceasiaa Queens itawakaribisha Bunda Queens kwenye Uwanja wa Samora mkoani, Iringa.

Mabingwa wa kwanza wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, Mlandizi Queens itakutana na Alliance Girls wakati Gets Program itawakaribisha Fountain Gate Princess kwenye Uwanja wa Kituo cha TFF ulioko Kigamboni.

"Nawaomba mpokee mabadiliko haya ya mechi kutokana na changamoto zilizoko nje ya uwezo wetu," alisema Mratibu wa Dawati la Soka la Wanawake la Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Bertha Matola.

Simba Queens yenye pointi 16 ndio mabingwa watetezi wa vinara wa ligi hiyo yenye kushirikisha timu 10.

# Michezo

Jumapili Desemba 15, 2024

Nipashe




Messi afunguka ubora wa Yamal UK. 21



Kiungo wa Yanga, Mudathir Yahya (kushoto), akiwania mpira dhidi ya nyota wa TP Mazembe, Josue Mungwengi katika mechi ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika Kundi A iliyochezwa kwenye Uwanja wa TP Mazembe ulioko Lubumbashi, DR Congo jana. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1.**PICHA: MTANDAO**

## Simba SC yatamba CS Sfaxien 'itakufa'

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA kuhakikisha wanazipata pointi tatu nyumbani, Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, ameahidi kubadili mfumo ili kuwafanya wachezaji wake wasichoke watakapowakabili CS Sfaxien ya Tunisia katika mechi ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Mechi hiyo ya raundi ya tatu ya Kundi A itachezwa kuanzia saa 10:00 jioni.

Fadlu alisema mchezo wa leo hautakuwa rahisi kwa sababu wapinzani wao pia wanahitaji ushindi ili kurejesha matumaini ya kusonga katika mashindano hayo yanayosimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Kocha huyo alisema wataingia uwanjani kwa tahadhari, lakini pia watacheza kwa kushambulia zaidi kwa ajili ya kutafuta mabao yatakayowawezesha kupata ushindi na pointi tatu.

Hata hivyo, alisema katika mchezo huo anatarajia kubadili mfumo wa uchezaji ili kuwafanya wachezaji wake wasichoke itakapofika kipindi cha pili, kama ilivyoonekana katika michezo kadhaa iliyopita ya hivi karibuni.

"Hii timu ni kubwa nchini Tunisia, ina wachezaji wazuri ambao ninawafahamu, lakini tunakwenda kucheza kwa kuhitaji ushindi, tutakwenda kucheza kwa kushambulia zaidi.

Imeonekana tunashindwa kuwa na kiwango kizuri kipindi cha pili, katika mchezo dhidi ya Bravo tulisababisha penalti kipindi cha pili, na hata mechi dhidi ya CS Contantine, tuliruhusu mabao kipindi cha pili mwanzoni, sisi kama benchi la ufundi tumekuwa tukilitafutia ufumbuzi.

Nadhani tunaweza kubadili mbinu ya uchezaji katika mechi hii ili wachezaji wetu wasichoke sana kipindi cha pili na kutowapa nafasi wapinzani kutushambulia sana," alisema kocha huyo.

Naye kiungo wa timu hiyo, Augustine Okejepha, amesema wamejiandaa vyema kuelekea mchezo huo.

"Tunaamini kwa kile ambacho tumekiandaa na kukipanga, mimi na wachezaji wenzangu tutawapa furaha mashabiki wa Simba, watakuwa na jioni nzuri," alisema Okajepha.

Simba iliyoko Kundi A, inashika nafasi ya tatu ikiwa na pointi tatu, ambapo kama itapata ushindi itafikisha pointi sita, huku ikisalia na michezo mitatu mingine.

# Dube aibeba Yanga Congo

## Bao lake la kusawazisha la jioni lainusuru na kichapo cha tatu...

**Na Adam Fungamwango**

BAO lililofungwa na Prince Dube dakika za majeruhi liliokoa Yanga kupata kipigo cha tatu mfululizo katika mechi ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya wenyeji TP Mazembe baada ya kupata sare ya bao 1-1.

**Wakati mashabiki kwenye Uwanja wa TP Mazembe wakiamini timu yao itaondoka na ushindi, krosi iliyopigwa na Nickson Kibabage, ilimkuta Dube ambaye aliunganisha kwa kichwa, mpira ukajaa ndani ya wavu na kuwafanya wasiamini kilichotokea.**

Kusawazishwa kwa bao hilo kulitokana na jitihada zilizofanywa na wachezaji walioingia kipindi cha pili, Dube aliyechukua nafasi ya Kennedy Musonda, Stephane Aziz Ki, aliyeingia badala ya Maxi Nzengeli, Clement Mzize, aliyechukua nafasi ya Mudathir Yahaya huku Duke Abuya akimpisha Mzambia Clatous Chama.

Yanga ilitawala zaidi mechi kipindi cha pili baada ya kufanya mabadiliko hayo, na ilionekana wangeweza kupata bao muda wowote, tofauti na TP Mazembe ambao pamoja na kwenda mbele mara chache, ilikuwa ikipata nafasi za wazi na kushindwa kuzitumia.

Awali Yanga ilitanguliwa kwa bao lililofungwa na Cheikh Fofana, aliyepigwa kichwa na mpira kugonga nguzo ya pembeni na kujaa wavuni licha ya Ibrahim Hamad 'Bacca' kuuokoa, lakini tayari mwamuzi aliashiria ulikuwa umevuka mstari.

Fofana alifunga bao hilo dakika ya 42, ikiwa ni dakika moja tu baada ya kuchukua nafasi ya Gloire Mujaya, aliyeumia.

Hata hivyo, matokeo hayo bado yanaifanya iendelee kushikilia mkia ikiwa na pointi moja kwa mechi tatu ilizocheza, baada ya kupoteza mechi mbili kwa kufungwa mabao 2-0 na Al Hilal Omdurman ya Sudan na baadaye ikachapwa na MC Alger huko Algeria.

Matokeo hayo bado yanaibakisha TP Mazembe katika nafasi ya tatu ikiwa na pointi mbili kufuatia sare ya bila kufungana waliyopata hapo nyumbani kwao walipowakaribisha MC Alger.

Yanga ilianza mchezo kwa kuonana kwa pasi fupi fupi, huku wachezaji wa TP Mazembe wakionekana kutoelewana vyema, pasi zao zikipotea na kuifanya mechi hiyo kutokuwa na hadhi yake.

Dakika ya pili tu, Yanga ilikuwa imeshalisalimia lango la wenyeji wao, baada ya Yao Kouassi kuambaa na mpira kwenye wingi ya kulia, aliingia ndani kidogo na kumpenyezea Kennedy Musonda, lakini wakati ajiandaa kufanya alichotaka, kipa Badara Faty, aliuwahi na kuudaka.

TP Mazembe ilijibu shambulio hilo dakika mbili baadaye, Magloire Ntambwe, alipowatoka mabeki wa Yanga, lakini shuti alilopiga lilitoka juu ya lango.

Kipa wa Yanga, Djigui Diarra, alifanya kazi ya ziada kudaka shuti la Boubakar Hanikoye aliyeupata mpira ndani ya eneo la hatari dakika ya 11 huku Mudathir alikaribia kuiandikia Yanga bao dakika ya 14, alipopiga shuti la mbali lililolenga lango, ambapo kama si uhodari wa kipa, Faty, hadithi ingekuwa nyingine.

Diarra, alilazimika kufanya tena kazi nyingine ya ziada dakika ya 28 alipokamata mkwaju wa Merceil Ngimbi, akiwa hatua chache tu kutoka alipo.

Shuti hilo lilisababisha kuumia na alitibiwa uwanja kwa muda mrefu, huku ilionekana kama hatoweza kuendelea tena kukaa langoni, lakini baadaye aliendelea.

Hakurejea tena kipindi cha pili na nafasi yake ikachukuliwa na Khomeiny Aboubakar, ambaye alisimama imara kuzuia hatari zote langoni mwake.

Timu hizo zitacheza mchezo wa raundi ya nne Januari 3, mwakani kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >